Jumanne Julai 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581746

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital


nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



**ØDEGAARD, JESUS NDANI ARSENAL ZIARANI MAREKANI**

UK. 21



**Wafugaji** waja na staili mpya kulisha mifugo shambani usiku

UKURASA 4



**Mtihani** ulivyo kwa mwenye ulemavu, ana watoto watatu, mwenyewe hajiwezi

UKURASA 5



**Mjue** mwanamama kijana Kamala Harris anayejiandaa kuvaa viatu vya Mzee Biden

UKURASA 19

RIPOTI MAALUM

# Mtego wa utapeli matangazo 'viwanja vinauzwa na hati'



• **Yamo** "Ukinunua viwili, unapata kimoja bureee"; serikali yatoa angalizo...

*Endelea Ukurasa 2*

## Bingwa adokeza kasi kiharusi kwa vijana inatisha

UKURASA 8

# Wadau: Nape, Makamba wameenguliwa na haya



Nape



January



Byabato

UK. 3

**MICHEZO** **YANGA YAWAONYA DUKE, ANDAMBWILE** UK.24 **MAONI,** UK.6



Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, aliyeongozana na viongozi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya akizungumzia tukio la kukamatwa kwa ng'ombe 20, waliodaiwa kukutwa kwenye mashamba ya wakulima Mvomero. **Habari kamili Uk. 4. PICHA: IDDA MUSHI**

Habari kamili Uk. 4.

# Mtego wa utapeli matangazo ya ‘viwanja vinauzwa na hati’

**Na Halfani Chusi**

“VIWANJA... viwanja... viwanja... njoo ujipatie kiwanja kilichopimwa na uanze kulipia kidogo kidogo; ukishamaliza unapewa hati papohapo!” Inasikika sauti kutoka katika spika ikitangaza biashara hiyo huko Kimara Darajani, wilayani Ubungo, mkoani Dar es Salaam.

Hivi sasa karibu kila palipo na makutano ya barabara za Dar es Salaam, mkoa wenye watu 5,383,728 sawa na asilimia 8.7 ya watu wote nchini kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, utakuta spika zikitoa sauti za matangazo yanayorudiwa kuhusu “viwanja vinauzwa”.

Kwenye spika hizo kuna namba za simu za kuwasiliana na wauzaji, huku wakihamasisha kuwa “ukinunua viwanja viwili utapewa kimoja bila malipo na utaratibu wa malipo umerahisishwa na “utalipa kidogo kidogo”.

Kuna jambo lingine la kuvuta wateja --, wanaotangaza wanasema, “Ukimleta mteja unapata Sh. 50,000 papohapo”.

Mbele za spika hizo za Kimara Darajani, mwandishi wa habari hii aliona bango lenye maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa yakisomeka “VIWANJA VINAUZWA KIBAHA KILUVYA SH. MILIONI 1.5, UNALIPA NUSU YA BEI HALAFU NYINGINE UNALIPA KIDOGO KIDOGO” yakifuatwa na namba za simu za kuwasiliana na wauzaji.

Chini ya bango hilo, mwandishi aliona watu waliokuwa wananakiri namba na baadhi yao walionekana kupiga simu papohapo.

Si Kimara tu, matangazo ya aina hii yameshika kasi jijini, huku kukiwa na angalizo aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kwamba wanaonunua viwanja hivyo wako hatarini kupoteza fedha zao kwa kuwa vingi ni vya matapeli na havina hati.

Silaa ambaye juzi usiku aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akichukua nafasi ya Nape Nnauye aliyetenguliwa, aliagiza viongozi wa wizara yake mwezi uliopita kushiriki kuondoa mabango yote yanayotumiwa kutangaza biashara hiyo.

Hata hivyo, wauzaji viwanja hivyo walipozungumza na mwandishi walijitetea kwamba siyo wote ni matapeli, bali wapo wachache miongoni mwao ambao siyo waaminifu, wanatumia mwanya huo kutapeli wateja.

Mwuzaji Viwanja George Kwezi anasema anafanya kazi kisheria na kampuni yake (jina la kampuni tunahifadhi) imesajiliwa na serikali; mteja anapomaliza kulipia kiwanja anapewa hati yake kutoka Wizara ya Ardhi.

“Kati yetu tunaouza viwanja wapo pia matapeli, lakini siyo wote tunaojihusisha na biashara ni matapeli, hapana! Tatizo lililopo ni kwamba sheria haibani matapeli. Mtu aliyebaka anabanwa sana kisheria kuliko tapeli wa viwanja,” analalama Kwezi.

Kuepuka migogoro ya ardhi na utapeli, Kwezi anasema kampuni yake ikipata eneo linalouzwa, wanakwenda ofisi za serikali ya mtaa husika kuangalia kama lipo katika ramani ya mipangomiji kabla ya kuanza kulitangaza kuliuza kwa wananchi.

Anaeleza kuwa baada ya hapo, huwa wanakwenda ofisi za manispaa husika kujiridhisha kuhusu uhalali wa kuuzwa kwa eneo husika, wakihusisha pia majirani wa eneo hilo.

Kwezi anasema kuwa baada ya kujiridhisha, mteja akishalipia hupimiwa eneo lake kisha wanakwenda Wizara ya Ardhi kufuatilia hati.

Hata hivyo, mteja Madee Suleimani, aliyenunua kiwanja kwa Kwezi, anadai alipomaliza kulipia kiwanja, aliambiwa asubiri kwa miezi kadhaa wafuatilie hati yake.

Madee anadai ni mwaka sasa tangu alipomaliza kulipia kiwanja chake pasi na kupewa hati ilhali awali aliaminishwa akimaliza kulipia atapewa hati ya kiwanja.

“Nimemaliza kulipia kiwanja changu Kibaha, wakati ninanunua niliambiwa nikimaliza kulipia kiwanja ninapewa hati, lakini kila nikidai ninaambiwa wana miradi mingi, hivyo niendelee kusubiri.

“Kibaya zaidi alituambiwa tunatakiwa kulipia Sh. 300,000 ili tupewe hati, jambo ambalo limezua taharuki kwetu sisi ambao tayari tumeshamaliza kulipia, hilo jambo (la malipo ya ziada) halikuwapo katika makubaliano ya awali,” analalama Madee.



Kwezi alipoulizwa na mwandishi kuhusu madai hayo, alikiri kutotoa hati kwa baadhi ya wateja wake, akijitetea kumetokana na kuwa na miradi mingi ya uuzaji, akisisitiza wawe na subira.

Kwezi pia anashauri serikali iweke adhabu kali kwa matapeli, ili kukomesha dhuluma ya ardhi ikwamo kufupisha muda wa kuendesha kesi za masuala ya ardhi mahakamani.

“Mtu akifungwa miaka 30 gerezani kwa utapeli, mwingine hawezi kurudia, shida iliyopo mtu anatapeli Sh. milioni 10 anafungwa jela miaka mitatu, hali kama hiyo inashawishi watu kufanya utapeli kwa kuona adhabu si kali,” anasema Kwezi.

Mwuzaji mwingine wa viwanja, Faustini Kibwana anasema wanaouza viwanja, wengi wao wanajulikana na serikali inawatambua. Wanaokamatwa kwa utapeli hawatoki kampuni zilizosajiliwa.

“Inawezekana japo sina hakika sana matapeli wa ardhi wapo na wanakuja kwa njia nyingi, si jambo la kututuhumu tu sisi tunaouza viwanja, kumbuka viwanja havinunuliwi kwetu tu, wapo watu binafsi na madalali, huko nako si salama.

“Serikali ingefanya ukaguzi kuangalia wanaoendesha kampuni za uuzaji viwanja bila kusajiliwa, maana hao ndio mzizi wa sisi sote kuonekana matapeli,” anasema Kibwana.

Katika uchunguzi wake, mwandishi pia amebaini wapo baadhi ya wananchi ‘wanaolizwa’ kwa kiwanja kuuzwa kwa watu wawili au zaidi, jambo ambalo huzua taharuki na migogoro.

Mkazi wa Goba, wilayani Ubungo, Simony Khamisi ambaye anadaiwa ni miongoni mwa waliowahi ‘kulizwa’ na mikasa ya aina hiyo inayofanywa na madalali wa viwanja, anasema kadhia hiyo iko zaidi kwa madalali wa kujitegemea ambao wanafanya kazi kwa karibu na maofisa ardhi, ambao hushirikiana nao kufanikisha utapeli.

Kutatua changamoto hiyo, Khamisi anasema wizara yenye dhamana ya ardhi ichukue hatua dhidi ya watumishi wake wanaojihusisha na utapeli wa aina hiyo unaoibua migogoro mingi nchini.

Rashid Luhale, mkazi wa Temeke, mkoani Dar es Salaam, anashauri serikali iweke bei elekezi ya viwanja kulingana na eneo na ukubwa, akiamini hatua hiyo itapunguza ulanguzi kwa wananchi.

“Hii itachangia wananchi wengi kumiliki ardhi na nyumba kuliko ilivyo sasa; walio wengi wanashindwa kutokana na changamoto zilizopo,” anasema Luhale.

Mwezi uliopita, Waziri Silaa baada ya kubaini kuwapo kesi nyingi za ardhi na malalamiko ofisini kwake, aliagiza mabango yaliyozagaa mitaani yakitangaza “viwanja vinauzwa” yaondolewa ndani ya siku saba.

Waziri huyo pia aliagiza kampuni zote zinazouza viwanja, ziweke dawati la mauzo ofisi za ardhi za wilaya na mikoa husika.

Silaa alitolea mfano mmoja wa walalamiaji aliyefika ofisini kwake kutafuta haki baada ya kuuziwa viwanja ‘hewa’ katika Manispaa ya Kigamboni na moja ya kampuni ambayo baada ya ufuatiliaji wake (waziri), alibaini kampuni tajwa (jina tunalo) ilikuwa imechukua Sh. milioni 116 kutoka kwa wananchi kama malipo ya viwanja ‘hewa’ walivyonunua.

“Huwezi kuuza kiwanja kwa ramani, kiwanja kinauzwa kwa hati, serikali haiwezi kukaa kimya wakati wananchi wanyonge wanateseka na kutapeliwa fedha zao,” Waziri Silaa alionya.

Aliwataka wenye kampuni za ardhi wanaotaka kuuza viwanja wakiwa katika ofisi zao, waombe hati za viwanja wanavyopima kabla ya kuviuza.

Waziri Silaa pia alielekeza makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa yote nchini kuharakisha mchakato wa utoaji hati kama zao la upimaji wowote wa ardhi.

Licha ya maagizo hayo ya Waziri Silla, matangazo ya “viwanja vinauzwa” yameendelea kusikika na kuonekana katika makutano ya barabara nyingi jijini.

HABARI KITAIFA

# Wadau: Nape, Makamba wameenguliwa na haya

**Na Mwandishi Wetu**

MJADALA mkali umeibuka kwenye mitandao ya kijamii baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kufanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri, wengi wakihoji kilichowaondoa mawaziri Nape Nnauye na January Makamba.

Wachambuzi wa siasa wamesema kilichofanywa na Rais Samia ni mabadiliko ya kawaida kwa kuwa ni suala la uwajibikaji, huku wengine wakihusisha na kauli za hivi karibuni za mmoja wa mawaziri hao.

Kwa mujibu wa wachambuzi hao, Rais amefanya mabadiliko ili kuboresha na kulisuka vyema Baraza la Mawaziri kuleta tija kwa Watanzania.

Waliondolewa na kuzua mjadala ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Pia yuko Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stephen Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini.

Licha ya Rais kutoeleza sababu za kutengua nafasi za mawaziri hao, baadhi ya watu walionesha kufurahia kuondolewa kwa Nape, wakielezwa kuchukizwa na kauli yake ya hivi karibuni kuhusu uchaguzi, waliyoitafsiri kukwaza ustawi wa demokrasia nchini.

Nape alisema kwamba matokeo ya uchaguzi hayategemei sanduku la kura bali nani anasimamamia uchaguzi na kuhesabu kura.

Safari ya uwaziri ya Nape ilianzia mwaka 2016, alipoteuliwa na Rais John Magufuli kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kudumu kwa muda mfupi, aliondolewa Julai 22, 2017.

Januari 8, 2022, Rais Samia alimrudisha Nape kwenye nafasi hiyo akiwa Waziri Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari hadi juzi usiku alipomtengua.

January alipoteuliwa na Rais Jakaya Kikwete kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia mwaka 2012 na kuitumikia nafasi hiyo kwa miaka mitatu hadi 2015.

Mwaka 2016, aliteuliwa na Rais Magufuli kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira na kisha kumwondoa katika nafasi hiyo Julai 21, 2019.

Septemba 2021, Rais Samia alimteua kuwa Waziri wa Madini na August 30, 2023 akamhamisha kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki hadi juzi usiku. Tangu mwaka 2010, January ni Mbunge wa Bumbuli, mkoani Tanga.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema alisema jana kuwa alitegemea viongozi hao, hasa Nape kuondolewa katika nyadhifa zao kutokana na kauli zao.

Alisema kauli ya Nape ya 'goli la mkono' ni hatari kwa nchi hiyo inayozingatia misingi ya kidemokrasia na uchaguzi huru, inatoa taswira ya kuwa kuwa hakuna demokrasia imara katika nchi.

Alisema demokrasia ndio njia pekee ya wananchi kuiondoa serikali iliyopo madarakani kama wakiona haifanyi vizuri, hivyo kauli hiyo inavua dhana hiyo iliyojengeka katika mawazo ya wananchi.

"Nape ni sehemu ya baraza la mawaziri, kutoa kauli kama ile ni hatari sana kwa demokrasia, serikali ni lazima ijenge taswira ya nchi kutegemea uchaguzi salama na wa haki," alisema Lema.

Mwanasiasa huyo pia alisema hakushangazwa kuondolewa kwa January kwa kuwa alitegemea kuona baadhi ya mawaziri wakitolewa, akitabiri hali hiyo pia kwa Waziri mteule wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba.

Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) - Shule Kuu ya Elimu, Dk. George Kahangwa alisema kilichotokea kwa viongozi hao kilitarajiwa na kuwa Nape alipaswa ajiuzulu mwenyewe kutokana na kauli aliyoitoa hivi karibuni kuhusu mshindi katika uchaguzi.

Kuhusu viongozi wengine waliotenguliwa, Kahangwa alisema ni kawaida kwa kuwa kiongozi anapoona wasaidizi wake hawaendani na kasi anayoitaka, anawajibika kuwaondoa na kuweka wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema alichokifanya Rais Samia ni alama ya uwajibikaji na uwajibishaji.

Juzi usiku, Rais Samia alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri. Mbali na mawaziri hao, Silaa ameteuliwa kushika nafasi ya Nape, huku nafasi yake ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikichukuliwa na Deogratius Ndejembi ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Rais Samia pia amemteua Ridhiwani Kikwete kuwa Waziri wa Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Kabla ya uteuzi huo, Ridhiwani alikuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Pia Rais amemteua Balozi Mahmoud Thabit Kombo kuwa Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Balozi wa Tanzania Italia.

Vilevile, Rais Samia amemteua Cosato David Chumi kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, akichukua nafasi ya Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk ambaye taarifa ya Ikulu ilieleza kuwa atapangiwa kituo cha kazi.

Saa chache kabla ya taarifa ya uteuzi mpya wa Rais Samia kutangazwa, Ofisi ya Bunge ilitoa taarifa kwa umma kuwa Balozi Mbarouk amemwandikia Spika barua kuomba kujiuzulu ubunge wa kuteuliwa na Rais.

Rais pia ameteua Deus Sangu kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, huku akimteua Dennis Londo kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki.

Taarifa ya Ikulu pia ilieleza kuwa Rais amemteua Eliakim Maswi kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), huku akimteua Mary Makondo kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma. Kabla ya uteuzi alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, anachukua nafasi ya Rehema Madenge ambaye amestaafu.

Kiseo Nzowa ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro. Kabla ya uteuzi alikuwa Ofisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais - Ikulu, huku Musa Haji Ali akiteuliwa kuwa Balozi. Kabla ya uteuzi alikuwa Ofisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais - Ikulu.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# BoT yakana kukiuka sheria matumizi Sh. trilioni 1.742/-

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) umetoa ufafanuzi kuhusu Sh. trilioni 1.742 zilizochukuliwa na serikali katika benki hiyo mwaka 2022/23, kwamba uko kisheria.

BoT imesema sheria iliyoiunda ya mwaka 2006 imeipa mamlaka ya kuipa serikali mkopo wa muda mfupi ili kuziba pengo au nakisi ya bajeti, hivyo hata kiasi tajwa hapo juu kilitolewa kwa msingi huo.

Imesema sheria hiyo inaisimamia BoT katika uendeshaji shughuli za serikali, ikiwamo kutoa huduma ya mikopo ya muda mfupi wa siku 180, lakini mkopo huo haupaswi kuzidi asilimia 18 ya mapato ya serikali kwa mwaka uliopita.

Mkurugenzi wa Huduma za Benki BoT, Agaton Kipandula, ndiye aliyetoa ufafanuzi huo jana jijini Dar es Salaam baada ya gazeti Nipashe Jumapili kuripoti kuhusu lilichokiita utata wa Sh. trilioni 1.7 kutolewa BoT.

Nipashe Jumapili iliripoti kuwa Sh. trilioni 1.742 zilizotolewa BoT katika mwaka 2022/23 na kutumiwa na serikali ilhali hazikuwa sehemu ya makusanyo ya serikali kwa mwaka huo wa fedha.

Akitolea ufafanuzi kuhusu fedha hizo, Kipandula alisema: "Benki Kuu ya Tanzania iko kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa kwake, Sura 197 na sheria tunayotumia sasa ni ya mwaka 2006.

"Kwa mujibu wa sheria hii, BoT ni benki ya serikali, hivyo fedha zote za serikali na mashirika au taasisi za umma zinatuzwa BoT."

Kipandula alisema sheria hiyo pia imetoa nafasi kwa BoT kutoa mkopo wa muda mfupi kwa serikali. Alisema mkopo huo kwa mujibu wa sheria unaitwa 'advance'; lengo lake ni kurekebisha kushuka na kupanda kwa mapato ya serikali.

"Kwahiyo, kupitia kipengele hicho, ndicho kinaifanya BoT ikopeshe serikali kwa muda mfupi. Sheria hiyo imeipa ukomo serikali wa kukopa ambayo ni asilimia 18 ya mapato yake.

"Mkopo huo ni wa 'offset fluctuation' (kuziba pengo/nakisi)). Kwa mfano, umekusanya Sh. 10,000 na unataka kulipa Sh. 15,000, ile Sh. 5,000 ndiyo inatengeneza mkopo. Na kadri siku zinavyokwenda kila mwisho wa mwezi serikali inarudi katika nafasi yake na kuwa sawa," alisema.

Kipandula alisema hata katika vitabu vya serikali, mkopo huo huwa hauonekani kwamba ilikopeshwa.

Alipoulizwa kama Bunge liliidhinisha serikali kupatiwa mkopo huo kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza, Kipandula alisema: "Bunge haliwezi kuidhinisha hili kwa sababu lengo si kutoa 'finance', serikali ina bajeti yake. Sheria ya Bajeti sisi BoT si sehemu ya mandate yetu, ipo chini ya Wizara ya Fedha."

Inaporejewa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 kuhusu suala hilo, inaonesha kuwa katika mwaka huo wa fedha, serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.880 ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 41.480 kwa Sh. bilioni 400.

CAG anafafanua kuwa kati ya Sh. trilioni 41.880 zilizokusanywa, Sh. trilioni 38.447 zilipokewa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, hivyo kuwapo tofauti ya Sh. trilioni 3.4334.

"Jumla ya matumizi yaliyofanywa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ili kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalikuwa Sh. trilioni 39.523 bila kujumuisha Sh. bilioni 665.80 zilizotolewa kama fedha zilizorejeshwa (refunds) na matumizi mengine kwenye jumla ya makusanyo ya Sh. trilioni 38.447, hivyo kusababisha nakisi katika Benki Kuu (BoT) ya Sh. trilioni 1.742 kufikia tarehe 30 Juni 2023," CAG anaeleza katika Ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu.

## Wafugaji wadaiwa kulisha mifugo katika mashamba ya wakulima

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

BAADHI ya wafugaji wilayani Mvomero, mkoani Morogoro wamebuni mbinu mpya ya kulisha mifugo katika mashamba ya wakulima kwa kuingiza mifugo shambani usiku.

Kutokana na hatua hiyo, uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi umeweka mkakati wa kuendesha doria za usiku kwa kushirikiana na wananchi ili kudhibiti kadhia hiyo.

Hatua hiyo imekuja baada ya kukamatwa kwa ng'ombe 20 wanaodaiwa wa mfugaji Taifa China, mkazi wa Dakawa, wilayani Mvomero wakiwa wameingizwa katika mashamba ya wananchi Julai 21, mwaka huu.

Mbali na mashamba ya wananchi, mifugo hiyo pia inadaiwa kuingizwa katika mashamba ya umwagiliaji yanayomilikiwa na Ushirika wa Wakulima wa Mpunga Dakawa (UWAWAKUDA) na mashamba ya mahindi katika bloku namba 19.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, alifika katika eneo hilo jana na kukemea hali hiyo, akitaka hatua za makusudi kuchukuliwa na polisi dhidi ya mtuhumiwa, ili iwe fundisho kwa wenye tabia ya aina hiyo.

Alisema kitendo cha wafugaji kutodhibiti mifugo yao na kuiacha kuzagaa kwenye mashamba ya wakulima nyakati za usiku, hakitofumbiwa macho kwa kuwa kinachochea ukosefu wa utu na ubinadamu na kurudisha nyuma maendeleo ya wengine ambao wanatumia nguvu na gharama kubwa kustawisha mazao yao.

Aliagiza kuwe na doria za kila mara kusaka mifugo inayorandaranda nyakati za usiku na itakayokamatwa ipelekewe ombi maalum mahakamani ili hakimu atoe kibali cha kutaifishwa.

"Huku kutozwa faini kila siku wanachukulia ni jambo jepesi na inawapa kiburi, na kwa vile wana fedha, wanaona ni kawaida tu, wanalipa na kulisha tena kwa mara nyingine, sasa ifike mahali hili la faini liishe na lije la kutaifisha mifugo," alionya Mkuu wa Wilaya.

Alitoa siku tatu kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kwa kushirikiana na polisi kuondoa kambi za mifugo jirani na skimu hiyo ya umwagiliaji, sambamba na mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli za ufugaji.

Mwenyekiti wa UWAWAKUDA, Charles Pangapanga alisema kwa kipindi kirefu wamekuwa na changamoto ya wafugaji kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima, pia wafugaji kuweka kambi jirani na mashamba hayo.

Alisema pamoja na maridhiano hayo, bado wafugaji wamekuwa wakikiuka na kuleta usumbufu mkubwa na wa mara kwa mara kwa kuingiza mifugo katika mashamba ya ushirika ambayo kwa umoja wake yana ukubwa wa ekari 5,000.

Wakulima wengine, Michael Sylvester, Salum Sekwao, Seleman Nassoro na Christina Juma, wote wa Dakawa, kwa nyakati tofauti walisema uingiaji holela wa mifugo shambani unasababisha hasara kubwa.

Mfugaji Taifa China ambaye ng'ombe 20 wamekamatwa kwa tuhuma za kuingia katika mashamba ya wakulima, alidai mifugo yake ilivunja zizi usiku na kuingia katika mashamba ya wakulima.


## NGOMENI ENTERPRISES

### RE ADVERTISED
### INIVITATION FOR TENDER CLOSED BIDS

We, **NGOMENI ENTERPRISES LIMITED** working on behalf of **CRDB BANK PLC** invites general public and interested buyers to submit closed bids for purchasing commercial cum residential landed properties belonging to Emmanuel Elisante & Frank Rwekiza Machume with details stated hereunder.

**DETAILS OF THE PROPERTY TO BE SOLD**

| SN | DESCRIPTION | REGISTRATION DETAILS | PHYSICAL LOCATION | DEADLINE OF SUBMISSION (DAY, DATE AND TIME |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Landed properties | Certificate of TitleNumber 82837, Land office No. 350952. | Located on Plot Number 109, Block "47", Kijitonyama area in Dar es salaam. | Tuesday, 06th August, 2024,before 10:30 Hours |
| 2. | Landed properties | Certificate of Security arrangement | Residential property | Tuesday, 06th August 2024,before 10:30 Hours |

**CONDITIONS AND REQUIREMENTS OF BID SUBMISSION**

1. The sale will be conducted through **OPEN COMPETITIVE TENDERING PROCESS.** The bids MUST be addressed and submitted during WORKING DAYS AND HOURS to NGOMENI ENTERPRISES LIMITED Office located at NEADA PLAZA, 2ND Floor,Kimara Temboni, Saranga Road, Ubungo District, Dar es Salaam City, Tanzania.
2. Bids should be submitted in sealed envelopes clearly marked **"PURCHASE OF A LANDED PROPERTY** and all closed bids shall be opened on Tuesday, 06th August, 2024, before 10:30 Hours at Our Office.
3. Upon receiving notification of award, the winner/buyer will be required to deposit 25% of the bid price within 24hours, whereas the remaining 75% will be paid within 14 days from the date of receipt of notification of award. Failure to pay the remaining 75% will result into forfeiture of the already deposited funds and the BID process will be repeated. All Payments should be made through CRDB Bank PLC account to be provided by **NGOMENI ENTERPRISES** and the Transfer shall clearly indicate name of the Bidder.
4. Any bidder will be required to fill in a prescribed form which shall be submitted as a bid declaration form, obtained at Our Office.
5. Interested bidders may inspect a property immediately after the publication of this advertising starting from 10:00 AM to 2:00 PM at own expenses including transport after consultation with Our Office.
6. Transfer of ownership charges and payment of relevant levies and taxes shall be borne by the successfully bidder.
7. The property shall be sold on the „as is where is basis.
8. Bids submitted after the set deadlines will NOT be received.

**CONTACT US FOR MORE DETAILS AND INQUIRIES THROUGH,
MANANGING DIRECTOR, NGOMENI ENTERPRISES, NEADA PLAZA BUILDING,
2ND FLOOR, KIMARA TEMBONI, SARANGA ROAD, ROAD, P O BOX 36359, DAR ES SALAAM
MOB:0753575752, Email: ngomenienterprises@gmail.com**



## KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)

### MWALIKO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA WAWEKEZAJI WATANZANIA WALIOSAJILI MIRADI KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC)

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ni Taasisi ya Serikali iliyo Chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliyoanzishwa Kwa Sheria ya Bunge Na. 26 ya mwaka 1997, iliyofutwa na kutungwa Sheria ya Uwekezaji Na.10 ya Mwaka 2022 Sura Na. 38 na kukasimiwa Jukumu la Kuratibu, Kuhimiza, kuhamasisha, na kuwezesha uwekezaji Nchini pamoja na kuishauri Serikali kuhusu Sera ya Uwekezaji na mambo mbalimbali yanayohusu Uwekezaji Nchini

Kituo Kinawaalika wawekezaji Watanzania/Wazawa waliosajili miradi ya Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kushiriki katika Mkutano huo muhimu wa Kimkakati utakaofanyika Siku ya Alhamisi tarehe 25 Julai 2024 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) uliopo jijini Dar es salaam kuanzia saa tatu 3:00 Asubuhi.

Malengo ya Mkutano huo ni pamoja na Kuwaelezea kuhusu maboresho mbalimbali yaliyofanywa na Serikali katika Mazingira ya Uwekezaji Nchini kupitia Sheria Mpya ya Uwekezaji Sura Na.38 ya mwaka 2022 na Kanuni zake, Kusikiliza Changamoto mbalimbali zinazowakabili wawekezaji katika Utekelezaji wa Miradi yao kwa lengo la kuzitafutia Utatuzi, na kuwashukuru wawekezaji Watanzania/Wazawa kwa kufanya Maamuzi Sahihi kuwekeza Nchini,.

Kwa Maelezo, Ufafanuzi na Uthibitisho wa Kushiriki, katika tukio hili muhimu na la kimkakati Usisite kuwasiliana na **Bi. Elizabeth Muzo kwa Simu 0712 461232 au barua pepe elizabeth.muzo@tic.go.tz**

*Karibuni Tujadili Uwekezaji Nchini*

# Wataka bajeti maalum ya huduma za uzazi kwa vijana

**Na Elizabeth Zaya**

JUKWAA la Utu wa Mtoto (CDF) kwa kushirikiana na Mtandao wa Vijana Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, wamesema kuna haja serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya utoaji huduma binafsi na rafiki za afya ya uzazi kwa vijana.

Wamesema licha ya jitihada na mafanikio ambayo serikali imepata katika eneo la afya ya uzazi, kumekuwa na changamoto mbalimbali, hasa za upatikanaji huduma rafiki za afya ya uzazi katika zahanati na vituo vya afya kutokana na upungufu wa watumishi wa afya, ukosefu wa miundombinu rafiki kwa vijana, zana za kisasa za matibabu na ukosefu wa mafunzo muhimu kwa watoahuduma wa afya.

Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Anold Massawe, Ofisa wa Programu wa CDF alisema:

“Katika eneo ambalo CDF inatekeleza mradi wa Youth Care, kwenye zahanati moja, kuna wastani wa watoahuduma ya afya wawili hadi wanne kwenye vituo vya afya wapo watumishi 25 hadi 30.

“Mwongozo wa uanzishaji vituo vya afya umeelekeza kituo cha afya kuwa na wastani wa watumishi 38 hadi 52 na zahanati watano hadi 11 kutokana na idadi ya wateja wanaowahudumia.

“Bado utekelezaji wake umekuwa na changamoto kwa vijana na wateja wengine kushindwa kupata huduma kwa wakati na hata wengine kukata tamaa ya kupata huduma na baadhi yao kutumia dawa za kienyeji kutokana na hofu kukaa muda mrefu katika vituo vya afya,” alisema.

Massawe alisema bajeti ya huduma ya mama na mtoto pekee inayotengwa na serikali, haitoshelezi utoaji huduma hususani katika kukidhi viwango vilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Taifa wa Viwango vya Huduma Bora za Afya kwa Vijana wa Mwaka 2020.

Alisema kutengwa bajeti hiyo ya utoaji huduma binafsi za afya ya uzazi kwa vijana, pamoja na mambo mengine, kutasaidia kutoa nakala za kutosha za mwongozo na kuzisambaza kwenye vituo vya afya, kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya ili kuwasaidia kutekeleza afua mbalimbali zilizopo kwenye mwongozo huo.

Pia alisema kutasaidia kununua bidhaa mbalimbali za huduma binafsi kama vile mipira ya kuzuia magojwa ya kuambukiza na kuzisambaza katika vituo vya afya, vifaa binafsi vya kujipima Ukimwi, vifaa vya kupima ujauzito na kutoa mafunzo maalum ya utoaji huduma rafiki kwa vijana kwa wahudumu wa afya.

Lingine Massawe alisema hatua hiyo itasaidia kutengeneza miundombinu kwa kutenga vyumba maalum vya utoaji huduma kwa vijana ili kutoa faragha na kupunguza ubaguzi na unyanyapaa katika vituo vya afya na hivyo kuwavutia wengi zaidi kujitokeza na kupata huduma binafsi za Ukimwi na afya ya uzazi.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia vijana kupata huduma bora, rafiki na salama zinazokidhi viwango, kujenga uhusiano wa kuaminiana kati yao na watoahuduma bila hofu ya kusikilizwa na wengine kwa sababu mazingira yasiyo salama yanaweza kusababisha kundi hilo kutopata au kuchelewa kutafuta huduma muhimu na hivyo kuongeza hatari ya matatizo ya kiafya.

“Kwa hiyo, ni muhimu kwa serikali na wadau wengine kuhakikisha huduma binafsi rafiki za afya ya uzazi kwa vijana zinazingatia viwango vyote ili kuboresha afya na ustawi kundi hili,” alishauri.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), kwa Tanzania mwaka 2021, huduma nyingi zinatolewa katika mazingira yasiyo rafiki na yenye faragha ndogo, jambo ambalo linaweza kuwakatisha tamaa vijana kutafuta huduma hizo.

“Huduma binafsi na rafiki za afya ya uzazi kwa vijana zinahitaji miundombinu maalum inayotoa faragha na mazingira mazuri kwa vijana, ambayo kwa sasa imekuwa changamoto kubwa kutokana na ukosefu wa bajeti ya kutosha.

“Hii inasababisha huduma kutolewa katika mazingira yasiyo rafiki na yenye faragha ndogo,” alisema Massawe na kushauri serikali itekeleze mwongozo kwa kuweka bajeti maalum na toshelezi katika eneo hilo la afya ya uzazi binafsi kwa vijana.

CDF kwa kushirikiana na Mtandao wa Vijana Wanaoishi na VVU wanatekeleza mradi wa miaka minne unaoitwa Youth Care katika Wilaya ya Tarime, mkoani Mara ukiwa na lengo la kuhakikisha vijana balehe wanaoishi na maambukizi ya VVU na mazingira hatarishi, hasa wasichana, wananufaika na sera wezeshi na mifumo imara ya upatikanaji huduma za afya ya uzazi na VVU.



Askofu wa Kanisa la Aglikana Tanzania, Dayosisi ya Rift Valley, John Lupaa, akimkabidhi msaada wa mahindi jana mmoja wa waathirika wa mafuriko, Maria Mussa, yaliyotokea Januari mwaka huu katika kijiji cha Sasajila wilayani Manyoni na kusababisha kaya zaidi ya 100 kukosa makazi na chakula. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Ajali ilivyobadili maisha ya Kahamba

## ●Wanawe walelewa kituo cha yatima

**Na Jenifer Gilla**

HUJAFA hujaumbika! Zakayo Kahamba (pichani chini), Mkazi wa Chanika jijini Dar es Salaam, aliyezaliwa na ulemavu wa miguu na baadaye kugongwa na lori, analalama kukabiliwa na hali ngumu ya maisha.

Kahamba (48) ni baba wa watoto watatu aliyekuwa anajishughulisha na biashara ya usafirishaji kwa kutumia Bajaji aliyopewa kwa mkataba wa miaka miwili.

Historia ya maisha yake ilibadilika zaidi Oktoba mwaka jana alipofika maeneo ya Kona ya Pugu- Ilala baada ya kupata ajali iliyotokana na kugongwa na lori na kusababishiwa majeraha ya kudumu katika mguu wake wa kulia.

Ajali hiyo iliharibu Bajaji aliyokuwa akiitegemea kuingiza kipato na kushindwa kufanya kazi, hali iliyomsababishia umasikini hata kushindwa kulea familia yake ya watoto watatu.

Kahamba alimweleza mwandishi wa Nipashe aliyefika nyumbani kwake kufahamu maisha mapya anayoishi kuwa dereva wa gari iliyogonga kwa pembeni Bajaji yake hakusimama baada ya ajali hivyo alikosa msaada wa kumkamata.

Akisimulia kwa majonzi, Kahamba alisema muda mfupi baada ya ajali, mkewe aliyekuwa akishirikiana naye kulea watoto alitoroka na kumwachia watoto ambapo hadi sasa hajui aliko.

“Nilichukua Bajaji ya mkataba, nikafanya kazi kama miezi miwili nikapata ajali pale Kona ya Pugu, kutokana na majeraha makubwa nilikwenda kutibiwa na niliikuwa nina watoto watatu nilioishi nao,” alisema.

Kahamba alisema kuwa baada ya ajali hiyo, kampuni iliyokuwa imemkopesha Bajaji ilichukua Bajaji hiyo kwa hoja kwamba kwa namna ilivyokuwa imeharibika isingeweza kuzalisha fedha.

Hata hivyo, walimweleza kuwa wangeirudisha atakapopona huku akiwa ndani ya mkataba wa mwaka mmoja na miezi nane.

Anaeleza kuwa baada ya kupona alikwenda kuichukua Bajaji hiyo, hata hivyo hawezi kuitumia kufanya biashara kwa kuwa haijafanyiwa marekebisho tangu alipopata ajali. Hivyo, wakaichukua tena baada ya kushindwa kulipa marejesho na kumwambia watairejesha kwake akilipa deni hilo.

“Niliitumia kama miezi miwili hivi ikawa inanisumbua kwa sababu haijafanyiwa marekebisho, kila siku ninakwenda gereji, nikawa ninashindwa kupata marejesho. Wakaja wakapiga hesabu nikawa ninadaiwa Sh. 266,000 wakaamua kuichukua,” alisema Kahamba.

Hivi sasa, kijana huyo anapitia hali ngumu kimaisha, akishindwa kulea watoto wake hata kutomudu kuwanunulia vifaa muhimu vya elimu kama sare za shule na madaftari.

“Baada ya kuona ninashindwa kutoa msaada huu kwa watoto, niliamua kuwapeleka Ustawi wa Jamii ili wapate msaada ndipo walipowachukua na kuwapeleka katika kituo cha kulea yatima kilichoko Chanika,” alisema.

Aliongeza kwa kusema kuwa wakati watoto hao wanachukuliwa, shule zilikuwa zimefungwa na baada ya kufunguliwa maofisa wa ustawi wa jamii walimweleza kuwa watoto hao wanatakiwa kuhamishiwa katika shule iliyoko karibu na kituo hivyo , alitakiwa atoe fedha kwa ajili ya kuwanunulia mahitaji muhimu.

Alisema kwa kuwa hakuwa na fedha hizo, watoto hao walishindwa kuhudhuria masomo kuanzia Januari mwaka huu mpaka Juni alipopatikana mdau na kugharamia mahitaji hayo.

“Yule Ofisa Ustawi wa Jamii baada ya kuona nimeshindwa kupata ile fedha aliamua kunipigania mpaka akapatikana huyo mdau wa kufadhili hayo mahitaji.

“Hivi sasa wanasoma darasa la nne, la tatu na la kwanza. Tangu wachukuliwe na ustawi wa Jamii sijawahi kuwaona hata siku moja kutokana na hali yangu duni kimaisha hivyo jambo hili linaniumiza kifikra,” alisema.

Aliomba serikali na wadau wengine kumsaidia angalau apate Sh. 266,000 ‘akakomboe’ Bajaji yake ili kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulea watoto hao na kulipa kodi ya nyumba.

“Nitashukuru sana kama atatokea mdau au Rais Samia Suluhu Hassan akaingilia kati kunisaidia angalau nipate hata nyumba ili niweze kuishi na familia yangu.

“Kule waliko wanangu ni sehemu ambayo wanalelewa watoto yatima hivyo wapo kama yatima ilhali Baba yao nipo. Hili linaniuma sana na ninatamani sana kuishi na wanangu,” alitamka kwa hisia kali.

Alisema kuwa yeyote anayeguswa na kilio chake, anaweza kumsaidia kupitia namba za simu: 0755380110 na 0616919855.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utekaji, mauaji watoto vilaaniwe

**KUMEJITOKEZA** matukio mfululizo ya utekaji, watoto kupotea au kukutwa wameuawa na kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali.

Mfululizo wa matukio haya unaleta tafakari kubwa kwa wazazi na walezi.

Hali hii pia imewaibua wadau wapenda haki za watoto na kulaani vitendo vya kutekwa, kuibwa na mauaji ya watoto, wakitaka serikali ichukue hatua kupambana na matukio hayo.

Wadau hao kutoka jijini Dar es Salaam, wameamua pia kuomboleza na kuwaombea watoto walioripotiwa kutekwa na kuuawa nchini hivi karibuni.

Vitendo hivi vilivyoibuka siku za karibuni vinatafakarisha na kuleta wasiwasi kwa jamii kwa kuwa kila mara lazima zipatikane taarifa za kupotea kwa watoto huku wazazi wakihaha kuwatafuta.

Wadau wamefikia hatua ya kuliweka suala hilo mikononi mwa Mungu kwa kufanya ibada ya kuwaombea watoto hao na kuwasha mishumaa kama ishara ya kukumbuka watoto hao.

Katika baadhi ya matukio yaliyowahi kutokea ni la Juni 3, mwaka huu, mkoani Kagera, ambapo mtoto Asimwe Novart, mwenye umri wa miaka miwili, alitekwa akiwa mikononi mwa mama yake na baadaye kukutwa amefariki dunia akiwa amenyofolewa baadhi ya viungo.

Julai 15, mkoani Dodoma, kuliripotiwa tukio la mtoto Sumaiya Issa, kutekwa na mpaka sasa hajapatikana; Julai 7, mwaka huu, huko Mbagala Dar es Salaam, mtoto Nusra Omari alikutwa ameuawa na baadhi ya viungo kunyofolewa; Julai 17 mkoani Dodoma, mtoto Theresphoa Mwakalinga alikutwa amefariki dunia na baadhi ya viungo vyake vimenyofolewa.

Mdau wa haki za watoto kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Getrude Dyabene, alisema anatambua jitihada zinazofanywa na serikali kulinda watoto, lakini wanasikitika kuona ukatili dhidi yao unaendelea.

Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), vitendo hivyo si tu kinyume cha haki za binadamu, bali pia ni kinyume cha Katiba ya Tanzania na sheria za nchi.

"Jeshi la Polisi limekuwa likitolea taarifa matukio ya aina hiyo, hata hivyo haturidhishwi na mikakati iliyowekwa ya ufutiliaji ili kukomesha vitendo hivyo.

"Kwa hali ilivyo sasa tulitarajia Jeshi la Polisi lifuatilie kwa umakini zaidi kujua chanzo cha haya matukio na wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua stahiki."

Wadau hao wamewasilisha hoja zao kwa serikali, na walimfikishia Rais Samia Suluhu Hassan, ambapo mdau kutoka Shirika la Msichana Initiatives, Rebeca Gyumi, alimwomba Rais kama Amiri Jeshi Mkuu, aendelee kusisitiza ulinzi na usalama wa mtoto.

"Taasisi zote zenye mamlaka ya ulinzi wa raia zitimize majukumu yake na kukamilisha kwa haraka uchunguzi wa kiini cha matukio haya na upelelezi kwa matukio yaliyotokea."


Kutoka Mtandao wa Haki za Watoto, Msafiri Mwajuma, ameshauri Jeshi la Polisi kufuatilia kwa haraka na kuweka kipaumbele taarifa za watoto kupotea bila kusubiri kupita saa 24.

Katika kufanikisha hilo, wazazi, walezi, jamii, walimu kwa ujumla wametakiwa kuongeza ulinzi kwa watoto na kuwahamasisha kutembea katika makundi, kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi katika jamii na kuwaelimisha watoto wasikubali kuambatana na watu wasiowafahamu.

Hizi ni baadhi tu ya hatua zinazoweza kusaidia watoto kutokumbana na matatizo hayo.

Kwa pamoja suala hili likifanyiwa kazi hakuna kitakachoshindikana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Joyce Lameck

# Zinahitajika zaidi shule za umma za Kiingereza

**MPANGO** wa kuanzisha shule za umma za Kiingereza hivi karibuni katika baadhi ya miji na majiji, unashika kasi.

Lakini kazi hiyo inapingwa na wadau mbalimbali wa elimu wanaoona kuwa huenda ukawa mwanzo wa kutengeneza matabaka kwenye elimu unaofanywa na serikali yenyewe.

Itakumbukwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, anatangaza mpango wa serikali wa kuanzisha shule zake zinazofundisha Kiingereza, unaolenga kuwapa wazazi machaguo wanayoweza kuyamudu katika kuamua hatima ya elimu ya watoto wao.

Aidha, anaeleza kuwa mpango huo unakuja na lengo la kuboresha ufundishaji wa Kiingereza, kwa sababu wamebaini kuna udhaifu mkubwa kwa wanafunzi kwenye kutumia lugha hiyo, baada ya kumaliza elimu ya msingi na kuendelea na sekondari.

Inavyoonekana ni kwamba kuwa na shule za mchepuo wa Kiingereza ni kutengeneza matabaka kwenye elimu ya umma, kwani serikali tangu uhuru imekuwa ikifundisha shule zake kuanzia darasa la awali hadi kidato cha sita sasa kwa Kiswahili.

Aidha, inatoa elimu kwa kutumia sera ya serikali kugharamia elimu bila wazazi kuchangia ada wala kutoa fedha kusomesha watoto wao mijini na vijijini.

Hata hivyo, kwenye shule hizi za serikali za Kiingereza, wazazi wamekuwa wakitakiwa kuchangia au kulipa Shilingi 400,000 ambacho hulipwa kila mwaka, kwa ajili ya kukidhi gharama za uendeshaji wa shule hizo.

Ikumbukwe serikali imeandaa utaratibu ambao inasema hautaleta usumbufu wa kulipa ada, pia kuathiri mzazi yeyote ambaye yupo karibu na shule hiyo na hakuna shule nyingine ya serikali ya Kiswahili, kwani atakubaliwa kumpeleka mtoto wake hapo.

Vile vile hata kama atamhamisha mtoto kwenye shule ya Kiswahili, hatalazimishwa kulipa ada katika shule zote za umma, zinazofundisha masomo yote kwa Kiswahili, katika ngazi ya msingi huku Kiingereza kikifundishwa kama somo na kuanzia ngazi ya sekondari na kuendelea.

Kwa mujibu wa wataalamu wa masuala ya elimu, matarajio ya mfumo huo yalikuwa kwamba miaka saba ya kufundishwa Kiingereza katika ngazi ya msingi, ni maandailzi ya kumfanya mwanafunzi aweze kufundishika na kuelewa masomo mengine katika lugha hiyo, atakapofika sekondari na vyuoni.

Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kwamba matarajio ya kuelewa Kingereza katika miaka ya awali hayafikiwi, katika kipindi cha walau miaka mitano iliyopita, takwimu za Baraza la Mitihani ya Taifa la Tanzania (NECTA) zinaonyesha kwamba zaidi ya wanafunzi wanaomaliza mitihani ya shule ya msingi huwa hawafaulu somo la Kingereza.

Hata katika matokeo ya mtihani wa ngazi ya Diploma ya Ualimu mara nyingi ufaulu huwa ni wa kuanzia kiwango cha daraja C kushuka chini, kwa mujibu wa takwimu tofauti zinazotolewa na wasomi na watafiti katika sekta ya elimu nchini.

Kama zaidi ya wanafunzi wanaoingia sekondari huwa hawajui Kiingereza, hii inaonesha kuwa wanakwenda kufundishwa masomo ambayo watapata taabu kuyaelewa, huu ndiyo msingi hoja ya wanaotaka lugha iwe Kiswahili kwa sababu ndiyo ambayo wanafunzi wanaielewa itumike sekondari.

Wanaotaka Kiingereza kipewe nafasi zaidi wanafanya hivyo, kwa hoja kwamba ndiyo lugha yenye maarifa na taarifa zaidi duniani kwa sasa, pia kuifahamu kunampa mwanafunzi wigo mpana zaidi wa kufanikiwa katika maisha yake ya sasa na badaye ikiwamo kupata fursa mpaka nje ya nchi.

Wanaoamini katika shule hizo wanasema zitasaidia wanafunzi kuingia kwenye ushindani wa elimu kimataifa, hivyo wanafunzi watapata fursa kutokana na kujifunza na kutumia Kiingereza.

Wanaopinga ujio wa shule za umma, wana haki ya maoni yao lakini ukweli ni kwamba muda au wakati ni sasa Watanzania kuungana na wadau wa elimu, ambao wameliona suala hili litaleta mabadiliko katika mfumo wa elimu nchini.

Kwa kutumia Kiingereza kufundisha kwenye masomo yote, kuanzia shule za awali, msingi, sekondari hadi watakapofikia hatua ya vyuo vikuu ni wazi itawapa ari, nguvu na uwezo kujiamini katika kuitumia lugha hiyo na kuinuka kimaisha.

# Atolewa uvimbe kilo 1.4 katika kizazi, aliishi nao miaka mitano

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MAMA wa watoto wanne, mkazi wa Siha, mkoani Kilimanjaro (jina tunalo), ametolewa uvimbe wenye uzito wa kilogramu 1.4 katika kizazi ambao ameishi nao kwa zaidi ya miaka mitano.

Uvimbe huo kitaalamu unaitwa 'mayoma' ulikuwa unaendelea kuota katika kizazi, huku ikielezwa ulikuwa na uwezekano wa kutokea ndani ya mfuko wa uzazi au pembeni mwa ukuta wa kizazi.

Akizungumzia upasuaji huo uliofanywa na jopo la madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Siha (DMO), Dk. Paschal Mbotta, alisema upasuaji huo uliochukua saa mbili na nusu, ulilenga zaidi kumwepusha mama huyo (44) na maumivu makali aliyokuwa akiyapata pamoja na kumwepusha kupata saratani ya kizazi.

"Tulikuwa na kambi ya siku tano ya madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake, ambayo tuliifanya kwa kutumia mapato ya ndani ya hospitali yetu ya Wilaya ya Siha.

"Sasa huyo mama alikuja tukamfanyia vipimo akaonekana ana tatizo la uvimbe katika kizazi. Alikuwa na upungufu wa damu, tukamwongeza damu na baada ya siku chache tukaingia naye katika operesheni.

"Sasa tulipoingia katika operesheni, tukakuta kitu kingine na tulichokiona kwenye vipimo vyetu. Ule uvimbe ulikuwa umekula kizazi chote na badala ya kuondoa hiyo mayoma peke yake ilibidi tuondoe kizazi chote; kwa sababu ilikuwa ni ngumu kutenganisha ule uvimbe na kizazi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mbotta, mama huyo hivi sasa anaendelea vizuri kiafya, Hospitali ya Wilaya ya Siha ikitoa huduma hizo za kibingwa kwa wananchi wake pamoja na wilaya jirani kuanzia Julai 15 hadi Julai 19 mwaka huu.




Meneja wa Programu ya Elimika, Khadija Ally (kulia), akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bagamoyo mkoani Pwani jana, inayolenga kuwaongezea uelewa kuhusu masuala ya afya ya uzazi, programu hiyo inatekelezwa na Taasisi ya Community Hands Foundation kwa ushirikiano wa Girlf First Initiative na Axio Consulting Group. **PICHA: MAULID MMBAGA**

Kambi hiyo ilihusisha madaktari bingwa wa upasuaji wa magonjwa ya kinamama (gynacologist) kutoka Hospitali Teule ya St. Joseph (Moshi), ikiongozwa na Dk. James Kimario na Dk. Peter Samweli kutoka Hospitali ya Faraja.

Dk. Mbotta alisema hakuna sababu maalum za kitaalamu zinazousababisha uvimbe huo, lakini tatizo kama hilo linatokea kutokana na historia ya familia, uzito mkubwa na wale wasiozaa (wagumba) au wanaotumia dawa za vichocheo.

# Mtoto aliyeibwa apatikana baada ya miezi mitano

**Na Shaban Njiia,** KAHAMA

MTOTO wa kike wa miezi tisa aliyeibwa katika Mtaa wa Nyihogo, Manispaa ya Kahama Desemba 9, 2023 amepatikana akiwa hai.

Imeelezwa na mamlaka za serikali kuwa mtoto huyo alipatikana Aprili 18 mwaka huu na kukabidhiwa Julai 18 mwaka huu kwa wazazi wake baada ya kuthibitishwa kwa vipimo vya vinasaba.

Mtoto huyo ambaye hivi sasa ana umri wa mwaka mmoja na miezi minne, alipatikana baada ya kutelekezwa na mwanamke aliyedaiwa kumwiba awali kwa kumlaghai dada yake kisha kutokomea naye kusikojulikana.

Baada ya kutelekezwa, aliokotwa na wasamalia wema ambao walimwona katika eneo la mtaa huo na kutoa taarifa kwa uongozi wa Serikali ya Mtaa wa Kisisi, ambao ulimpeleka katika ofisi za Ustawi wa Jamii.

Akithibitisha kupokea mtoto huyo na kumkabidhi kwa wazazi wake, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri hiyo, Alinda Bwakea, alisema jana kuwa baada ya kuokotwa, mtoto huyo alipelekwa ofisini kwao na viongozi wa Serikali ya Mtaa kwa kufuata taratibu zote za kisheria.

Alisema kuwa baada ya kuokotwa, waliwasiliana na watu waliokuwa wametoa taarifa ya kupotea kwa mtoto na waliojitokeza walipimwa vinasaba vyao (DNA) ili kubaini kama ni mtoto wao.

Ofisa huyo alisema kuwa majibu yalitoka kuwa ni mtoto wao ambaye aliibwa na walikuwa wakimtafuta kwa kipindi chote hicho.

Bwakea alitoa wito kwa wazazi, walezi na familia nyingine kuwa makini zaidi katika suala la ulinzi wa watoto kwa wanaowalea au kucheza nao pale wanapoona mtu wasiyemfahamu - wanarubuniwa kwa kuwapatia chochote, soda na pipi zikiwa sehemu ya mtego wa wahalifu kunasa watoto.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Rose Medadi akisimulia tukio na namna alivyoibiwa mtoto wake, alisema kuwa siku hiyo mwanawe alikuwa amebebwa na dada yake wa miaka saba wakiwa mazingira ya nyumbani, walikutana na mwizi huyo aliyewatuma wakamletee vocha dukani na kumwachia mtoto.

"Ninakumbuka maelezo ya mwanangu kuwa alitumwa vocha dukani na mama mmoja ambaye hakumtaja jina kwa kumpatia Sh. 2,000 na akamwomba ampatie mtoto kwa madai ya kuwahi na alifanya hivyo bila woga na aliporejea hakumkuta mama huyo alipomwacha," alisimulia.

Baba wa mtoto huyo, Paschal Ng'ondi alisema kuwa baada ya kufikishiwa taarifa za kuibwa mtoto wake huyo aliarifu uongozi wa serikali ya mtaa na Jeshi la Polisi na kuanza jitihada za kumtafuta.

Alisema kuwa April 18 walipata taarifa za kupatikana kwa mtoto huyo na kwenda moja kwa moja ofisi za Ustawi wa Jamii.

Alisema kuwa kutokana na kumfahamu vyema mtoto wao walipofika, walimtambua ni mwanawe lakini kulihitajika kufuatwa taratibu za kisheria ikiwamo kupima vinasaba na vilipokamilika walikabidhiwa mtoto wao na wanaendelea na malezi, wakitaka wazazi wengine kuwa makini na watoto wao.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# NEMC yatoa cheti cha Tathmini ya Mazingira miradi 9,000

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa Cheti cha Tathmini ya Mazingira (EIA), kwenye miradi 9,000 yenye thamani ya Sh. trilioni 40 ndani ya kipindi cha miaka mitatu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, wakati akizungumza na uongozi na wafanyakazi wa baraza hilo alipokwenda kuwaaga Mikocheni baada ya kuteuliwa kwenye nafasi mpya.

Alisema moja ya mafanikio makubwa anayojivunia ni baraza hilo kutoka kwenye utoaji wa huduma katika mfumo wa analojia na kwenda kidijitali ambako kumerahisisha utoaji wa huduma kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Alisema zamani alikuwa akitia saini vyeti vya EIA kwa mfumo wa analojia, lakini baada ya mageuzi makubwa sasa vinatolewa kidijitali hali ambayo imeondoa usumbufu kwa wawekezaji wanaofika kwenye baraza hilo.

"Zamani cheti cha EIA kilikuwa kinazunguka sana, lakini leo hii waziri akishasaini tu kinakuwa tayari kwa ajili ya kuchapishwa na mwekezaji anapata ndani ya muda mfupi kwa hili nawapongeza sana na endeleeni kuboresha mifumo dunia inakwenda kidijitali," alisema.

"Tumefanikisha uwekezaji wa karibu miradi 9,000 wenye thamani ya trilioni 40 sio jambo dogo, mnafanyakazi kubwa sana mmesaidia sana na ukiangalia NEMC imebadilika sana sio ile ambayo ilikuwa inalalamikiwa kila wakati," alisema.

Aidha, Jafo alisema NEMC imesaidia kuhamasisha wananchi kufahamu umuhimu wa miti na kwa sasa vijana wengi wamejiajiri katika biashara ya kuuza mbegu za miti kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema akiwa kwenye wizara ya mazingira, alifanikiwa kushirikiana na baraza hilo kupambana na uchafuzi wa mazingira ikiwamo kukomesha utiririshaji wa maji taka unaofanywa na baadhi ya viwanda.

"Tumefanya pamoja kama timu na kwa kuheshimiana ndio sababu tumefika hapa tulipo na naomba mafanikio haya yalindwe kuhakikisha mazingira yanatunzwa na turithishe vizazi vijavyo mazingira bora," alisema.

Aliutaka uongozi wa NEMC kuwawekea mazingira mazuri wafanyakazi ili wawe na motisha wa kufanyakazi akisema kuwa mtu mwenye msongo wa mawazo hawezi kufanyakazi kwa ufanisi.

"Msiwadharau madereva, wahudumu wa ofisi kwasababu wote hatuwezi kuwa wakurugenzi lazima ofisi iwe na watumishi wa kada mbalimbali kwa hiyo mdogo amheshimu mkubwa na mkubwa amheshimu mdogo pia," alisema Jafo.

"Ukiwa kwenye nafasi ya uongozi usiwaumize wenzako kwa sababu huwezi kujua huyu ambaye unamdharau kesho atakuwa nani, ishi kwa nidhamu na kuheshimu kila mtu kama akiba yako itakayokusaidia siku za baadaye," alisema Waziri Jafo.

Alisema wanapaswa kusimamia kikamilifu sheria, taratibu na kanuni ili kuiweka nchi kwenye mazingira mazuri na kuwasaidia wawekezaji kufanya shughuli zao bila kusubiri kwa muda mrefu kupata huduma wanazotaka.

Mkurugenzi Mkuu wa (NEMC), Dk. Immaculate Semesi, alisema kwa muda waliokuwa pamoja NEMC imefanikisha kusimamia uzingatiaji wa mazingira na walifanya kaguzi 3,000 za mazingira kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Tumeendelea kusimamia zuio la matumizi ya mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku ambapo zaidi ya tani 90 ilikamatwa na kutaifishwa na kuzuia utupaji ovyo wa taka hatarishi na vibali zaidi ya 1,000 vya usafirishaji wa taka hizo vilitolewa na baraza," alisema.




Wanaharakati wa haki za watoto wakiwa na mishumaa katika maombolezo ya utekaji na vifo vya watoto, yaliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Kijitonyama Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Treni ya umeme Dar-Dodoma kumekucha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma umekamilika kwa asilimia 99, huku safari za treni zikitarajiwa kuanza kesho.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa alisema hivi sasa wanaendelea kukamilisha vitu vichache ili ifikapo Julai 25, mwaka huu safari zianze rasmi.

"Hivi sasa tumefikia asilimia 99 na wataalamu wetu wanamalizia vitu vichache ili safari zianze rasmi siku ya Alhamisi Julai 25 mwaka huu. Tumeweka utaratibu mzuri kwa wananchi kukata tiketi kwa njia ya mtandao ili kurahisisha mambo.

"Baada ya kukamilisha kazi zote, wizara inaendelea kuweka utaratibu ili Rais Dk. Samia aweke jiwe la msingi la kuzindua rasmi safari za treni ya mwendo kasi," alisema.

Kadogosa aliomba viongozi wa kimila kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji miundombinu ya SGR kwa kuwa serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia ujenzi wake.

"Viongozi wa kimila, wakiwamo machifu, ni muhimu hasa katika ulinzi wa miundombinu ya reli. Niendelee kuwaomba ndugu zetu mwendelee kutoa elimu kwa wananchi faida ya reli hii hasa katika kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla," alisema.

Chifu wa Dodoma, Mazengo wa Pili, alipongeza serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa ya kimkakati, ukiwamo ujenzi wa reli hiyo ambao kukamilika kwake kutafungua nchi kiuchumi.

Alisisitiza wananchi wanaozunguka miradi mikubwa ya kimkakati kuendelea kutumia fursa zinazopatikana katika maeneo yao kujikwamua kiuchumi.

# 'Kiharusi hatari kwa mfumo wa fahamu'

**Na Christina Mwakangale**

BINGWA Mbobezi wa Mfumo wa Fahamu (Neurologist) kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Henrika Kimambo, amesema miongoni mwa magonjwa yanayokua na kuathiri zaidi mfumo wa fahamu ni kiharusi.

Amesema takwimu za wanaougua ugonjwa huo, zinaongezeka wakiwamo vijana wenye umri kati ya miaka 20 huku kwa siku wanaohudhuria kliniki hospitalini hapo wakiwa na changamoto ya mfumo wa fahamu ni takribani 100 hadi 200, wengi wao wenye kiharusi.

Aliyasema hayo hivi karibuni, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu mfumo wa fahamu, kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), katika Banda la MNH.

"Mfumo wa fahamu ni mpana ni mtandao kama umeme tangu pale unaozalishwa hadi kufika mtumiaji. Mfumo wa fahamu si kiungo kimoja, lakini hapa tunauzungumzia ubongo ambao una mwendelezo hadi kwenye uti wa mgongo.

"Kisha uti wa mgongo una mishipa ya fahamu kwenda maeneo tofauti kichwani, kifuani, miguuni, mikononi kote huku taarifa zinapokelewa kwa muda mfupi sana, kama vile ukichomwa na mwiba taarifa itakwenda nimechomwa.

"Taarifa za hisia zinasafirishwa na ubongo unatafsiri kwa sekunde. Baridi, joto, njaa, ulimi unabaini ladha. Masikio, pia vyote vinategemea mfumo huu na ubongo unatafsiri," alisema Dk. Henrika.

Alisema inapotokea changamoto katika mfumo eneo lolote katika ubongo au uti wa mgongo, taarifa hushindwa kutafsiriwa kutokana na ajali, mshipa kuziba ama donge la damu kuziba katika ubongo.

"Kwa nyakati hizi changamoto ni kiharusi, ambao unaathiri ugonjwa wa fahamu nchini. Idadi inakuwa kubwa, zamani walikuwa wagonjwa watu wazima, lakini sasa kuna walio na umri wa miaka 30 hata 20.

"Sababu za kiharusi kwa vijana hao unakuta ni zilezile za watu wazima wanaougua. Kutokana na mtindo wa maisha kubadilika, hakuna mazoezi, mlo, sasa magonjwa yasiyoambukiza (NCDs), ndio yameshika kasi," alisema bingwa huyo.

Alisema wagonjwa wengi wanaofika hospitalini hapo ni kiharusi katika ubongo, kutokana na sababu tofauti kama vile damu kuziba mishipa, kupasuka, presha na kusababisha uwezo wa kufanya kazi ni mdogo.

"Sababu nyingine zinazosababisha kiharusi ni kurithi, wenye VVU, walio na 'cholesterol' na kutofanya mazoezi. Inapotokea tatizo mgonjwa awahishwe hospitalini," aliongeza Dk. Henrika.

Alisema kliniki ya mfumo wa fahamu mara tatu kwa wiki, inayofanyika hospitalini hapo inahudhuriwa pia na wenye tatizo la mgongo, kifafa na miguu.



# Makundi ya mifugo kutoka Kenya yavamia malisho

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

MAKUNDI makubwa ya mifugo inayodaiwa kuingia nchini kinyemela, yamevamia nyanda za malisho zinazolizunguka Ziwa Natron lililopo wilayani hapa Mkoa wa Arusha kutafuta malisho.

Uvamizi huo uligundulika juzi baada ya wadau wa mazingira nchini, Shirika la World Wildlife Fund (WWF), kutembelea nyanda hizo za malisho na kukumbana na kilio cha jamii za wafugaji wa Kimasai.

Akizungumzia uvamizi wa mifugo hiyo inayodaiwa kuingia nchini kupitia vichochoro vya mpakani wilayani hapa, ikitokea nchi jirani ya Kenya, mmoja wa wafugaji hao, Mericiana Benders, aliiomba serikali kuchukua hatua haraka kunusuru nyanda hizo kuharibiwa na mifugo.

"Hizi nyanda za malisho kuzunguka Ziwa Natron, ndio tegemeo letu wakazi wa vijiji vilivyoko ukanda huu. Sasa kuna makundi ya ng'ombe na mbuzi kutoka Kenya yanaingia kinyemela vijijini kutafuta malisho. Tunaomba serikali itusaidie kuwaondoa na kuzuia kuingia kwenye nyanda za malisho," alisema mfugaji mwingine wa Longido, Paulo Laizer.

Mbali na mifugo hiyo kutoka Kenya, nyanda hizo zimevamiwa na mimea vamizi na kutishia kutoweka, ustawi wa mazingira kuwa hatarini na kuleta athari kwa malisho ya wanyama na viumbe wengine.

Meneja Mradi wa Mazingira wa WWF, Gasto Mushi, alisema wameanzisha mkakati wa kunusuru nyanda hizo kuvamiwa na mimea vamizi kwa kuja na mradi wa REDAA, utakaotoa elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima na wafugaji.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi, akizungumza na wadau hao, alisema serikali inaunga mkono juhudi za wadau wa mazingira wanaofanya juhudi za kuokoa mazingira na ikolojia.

Kwa mujibu wa Ng'umbi, serikali imepokea kilio cha wafugaji hao kuhusu uvamizi wa mifugo na kusisitiza haitawavumilia wanaosababisha uharibifu wa mazingira.




Mkuu wa Kitengo cha Polisi Usalama Barabarani, Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, ASP Leonard Bandola (kushoto), akiagana na Mkaguzi wa Polisi, Patrick Masawe, baada ya kutoa maelekezo ya kazi katika stendi kuu ya mabasi Muheza kuhusu ukaguzi na utoaji elimu kwa abiria, madereva kufuata sheria kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani pamoja kukagua stika. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Aweso azungumzia mita za LUKU za maji

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso amesema matumizi ya mita za luku kwa kulipia nkara za maji utakuwa mwarobaini wa malalamiko sugu ya wananchi nchini kubambikiwa malipo.

Aweso aliyasema hayo juzi wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba ya utekelezaji wa mradi wa hatifungani jijini Tanga.

"Lazima tukubali sasa kama Wizara ya Maji, teknolojia zitumike kufanya mageuzi kwenye sekta ya maji, hatuwezi kukubali kila kukicha mwananchi analalamika amebambikiwa bili ya maji,

"Luku za maji zitumike kwani ndiyo uelekeo sahihi, hatutamvulia Mkurugenzi au Mtendaji, ambaye hatachukulia uzito wa huduma hii kwa kuona siyo mwelekeo sahihi," alisema.

Waziri huyo ameitaka Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi, Taka na Mazingira (UWASA) Tanga kushirikisha jamii na viongozi wa maeneo ambayo wanakwenda kuweka miradi ili kufanya kazi zao kwa uhakika na kukamilisha miradi hiyo.

"Jamii ipo na viongozi wapo ukiwashirikisha utafanikiwa na usipowashirikisha utakwama, wakati mwingine taasisi zinakwama kwa kutowashirikisha viongozi, utakuta mnaenda kwenye ukaguzi wa mradi lakini hata mtendaji wa eneo husika hayupo, hii siyo sawa," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Tanga UWASA, Geoffrey Hill, alisema mradi huo una lenga kuboresha huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka hiyo.

"Mradi huu pia upo kwenye kutekeleza agizo la Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuwa umelenga kupunguza malalamiko ya wateja wetu kwa kufunga dira janja za malipo ya kabla ambapo mteja atapata maji kulingana na malipo yake, hakuna kudaiana wala kubambikiana bili," alisema Hill.

Alisema awali walilenga kufunga mita za maji za luku zipatazo 10,000 lakini kupitia mradi huo, wamepata mita nyingine 4,000, ambazo zitaanza kufungwa kwa wateja mwezi huu.

Alisema mradi huo pia umelenga kuongeza uzalishaji wa maji na kuwanufaisha wakazi wa wilaya za Tanga, Muheza, Pangani na Korogwe.

"Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 53.12 na unatazamiwa kukamilika kipindi cha miezi 15 mpaka kufikia Oktoba mwaka 2025," alisema.

# Wachimba madini waivuta serikali Mirerani, yajenga kituo cha afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

SERIKALI inajenga kituo cha afya eneo la Mirerani mkoani hapa baada ya kupata msukumo wa kuwapo idadi kubwa ya migodi na wachimbaji wa madini ya tanzanite na kupunguza adha kufuata huduma za matibabu wilaya jirani.

Kituo hicho kilichopewa jina la 'Tanzanite' kinajengwa na serikali kuu katika eneo hilo kwa gharama ya Sh. milioni 500.

Jana, Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk.Namnyaki Lukumay, alisema kituo hicho kitakuwa na jengo la wagonjwa wa nje, maabara, jengo pacha la wazazi na upasuaji.

"Ujenzi wa Kituo cha Afya Tanzanite, ulianza Machi 22, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika kabla ya Oktoba mwaka huu.

"Lengo la kujenga kituo hiki ni kutimiza azma ya serikali ya kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali mbalimbali na kuzidi kusogeza huduma bora za afya kwa karibu na jamii ya mji mdogo wa Mirerani," alisema Dk. Lukumay.

Diwani wa Kata ya Mirerani, Salome Mnyawi, aliishuku serikali kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Salome, alisema kituo hicho pamoja na kuwasaidia wakazi wa kata yake, kitapunguza msongamano kwenye Kituo cha Afya kilichopo Kata ya Endiamtu.

"Nawapongeza mno viongozi wa kamati ya ujenzi wakiongozwa na Mwenyekiti wao mdau wa maendeleo, Taiko Ole Kulunju na Katibu wake, Charles Nyasuka kwa usimamizi mzuri na wakizalendo," alisema.

Alisema Taiko na Nyasuka, wamekuwa chachu ya maendeleo, kwa kutoa fedha zao binafsi mfukoni ujenzi unapokwama ili uendelee.





# Mchungaji mbaroni kwa mauaji, wizi wa gari

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani hapa, limemkamata na kumfikisha mahakamani aliyekuwa Mchungaji wa Kanisa la T.A.G Kata ya Buhongwa, George Masangya, kwa tuhuma za mauaji ya Majuto Seif na wizi wa gari.

Hayo yalisemwa juzi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa wakati akizungumzia kuhusu kukamatwa kwa watu 179 kwa tuhuma za mauaji, wizi, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Mutafungwa, alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika msako uliofanywa na jeshi hilo dhidi ya uhalifu kwa kipindi cha mwezi mmoja maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Alisema mtuhumiwa Masangya, alikamatwa kwa tuhuma za mauaji hayo yaliyotokea Juni, 28 mwaka huu wilayani Ilemela na wizi wa gari hilo.

Alisema baada ya askari wa jeshi hilo kukamilisha upelelezi dhidi ya mtuhumiwa huyo, walimfikisha mahakamani kujibu mashtaka ya mauaji.

Akizungumzia kuhusu tukio jingine, alisema wanamshikilia mkulima, Lupande Ngw'andu (43), Mkazi wa Kijiji cha Kasela kwa tuhuma za kumuua Mwajuma Yugele kwa kumpiga na kitu kizito kichwani kutokana na wivu wa mapenzi.

Alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya mauaji hayo Julai 13, mwaka huu majira ya saa 11:00 alfajiri katika kijiji hicho kilichoko Kata ya Nyakalilo Wilaya ya Sengerema na kutoroka.

"Baada ya ufuatiliaji Julai 16 majira ya saa 02:00 asubuhi tulifanikiwa kumkamata mtuhumiwa akiwa amejificha katika Kijiji cha Busango Kata ya Segese Wilaya ya Msalala mkoani Shinyanga," alisema Mutafungwa.

Akizungumzia kuhusu matukio mengine, alisema wanawashilikia watu 39 kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kilo 14.2 za kulevya aina ya bangi.

Alisema watuhumiwa wengine 63 waliwakamata baada ya kukutwa na lita 1,345 za gongo na mitambo mitano ya kutengenezea pombe hiyo hiyo haramu.

Mutafungwa, alisema watuhumiwa 63 walikutwa na vifaa vya kupigia ramli chonganishi na wawili mtambo wa kutengenezea barabara.

Alisema katika msako huo, jeshi hilo, limekamata vielelezo zikiwamo deki tatu na pikipiki tano aina ya TVS, Sunlg, Bajaji na Kinglion mbili mali zinazodhaniwa kuwa ni za wizi.

"Baadhi ya watuhumiwa tumewafikisha mahakamani huku wengine wakiendelea kusubiri upelelezi wa kesi zao, pindi utakapo kamilika watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka," alisisitiza Mutafungwa.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Kailima Ramadhani, akimkabidhi kadi ya mpigakura, Hanifa Chija, mkazi wa Mtaa wa Boma Kata ya Kimobwa, wilayani Kasulu mkoani Kigoma, baada ya kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Mpigakura katika kituo cha Ofisi ya Mkuu wa Wilaya mwishoni mwa wiki. **PICHA: INEC**

# Raia wa Burundi matatani kuingia nchini kinyemela

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

IDARA ya Uhamiaji wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, inawashikilia raia 29 wa Burundi kwa tuhuma za kuingia kinyemela na kuishi bila ya kuwa na vibali.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Kahama, Salum Rashid, watuhumiwa hao wenye umri kati ya miaka 13 hadi 17 walikamatwa juzi katika maeneo ya kata za Manispaa ya Kahama za Majengo, Nyihogo na Kagogwa wakijihusisha na biashara ndogo ndogo za mayai, karanga huku wengine wakiwa wameajiriwana Watanzania kuuza bidhaa hizo nakuchunga mifugo.

Rashid alisema kuwa baada ya watuhumiwa hao kuhojiwa, walidai wameingia kinyume cha sheria kuja kutafuta maisha kutokana na hali ngumu nchini kwao.

Alisema kila mwezi maofisa hao wa idara hiyo wanawakamata wahamiaji haramu 50 mpaka100 hasa watoto kutoka nchi za Rwanda, Burundi, Kenya na Ethiopia.

Rashid alisema baada ya watuhumiwa hao kuhojiwa, watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka na kwamba wakipatikana na hatia, adhabu kwa kila mmoja ni fani ya Sh. milioni tano hadi 20 ikiambatana na kifungo jela.

Mkaguzi Msaidizi wa Uhamiaji, Nicodemas Chagoma aliitaka jamii kutoa taarifa kwa jeshi hilo wanapowaona watu wanaowatilia ili sheria ichukue mkondo wake.

Chagoma aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuwamiliki wahamiaji haramu bila ya kufuata sheria, vingine watakaokabainika watakamatwa na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

# Wagawiwa mbegu mpya za michikichi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAKULIMA wa mikoa ya Tabora na Katavi wanatarajia kuanza kunufaika na mbegu mpya ya mchikichi ya Tenera inayokomaa ndani ya kipindi kifupi cha miaka mitatu.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu Tawala wa Wilaya ya Tanganyika, Lincoln Tamba, wakati akikabidhi miche 3,000 ya mbegu hiyo kwa wakulima katika hafla iliyofanyika Chuo cha Utafiti wa Kilimo Tumbi, mkoani hapa.

Tamba, alisema mbegu hiyo ambayo imefanyiwa utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kihinga mkoani Kigoma na TARI Tumbi mkoani Tabora, itawezesha wakulima kupata manufaa kwa muda mfupi.

Alisema mbegu hiyo itawawezesha kuondokana na umaskini, kuinua uchumi wao na kuwataka kuanza kutumia kwa kuzingatia elimu na kanuni za kilimo bora chenye tija na manufaa.

Mkurugenzi wa TARI Tumbi, Tabora, Dk. Emmanuel Mrema, alisema tangu kuanza kwa utafiti huo hadi sasa miche milioni 15 ya mbegu bora zimeshasambazwa kwa wakulima.

Mrema, alisema miche milioni 3.8 ya Tenera imesambazwa katika mikoa ya Tabora na Katavi.

Wakulima wa zao hilo, Mohamed Kalembe na Deus Kakola wa Wilaya za Nsimbo na Tanganyika miongoni mwa waliogawiwa miche hiyo, walisema itawaongezea uzalishaji wa zao hilo.

# DED akemea uchafu vituo vya afya

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, Binuru Shekidele, amekea kukithiri kwa uchafu katika vituo vya afya vilivyoko katika halmashauri hiyo na kuwaagiza watumishi wa Idara ya Afya kutekeleza ipasavyo majukumu yao.

Shekidele alitoa agizo hilo juzi baada ya kukagua utoaji wa huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Mwabaruhi na vituo vya afya vya Buzilasonga na Nyamazungo.

Alisema watumishi hao wanapaswa kulinda rasilimali zilizopo katika vituo hivyo, kutoa huduma bora kwa wananchi na kuzingatia usafi kwenye maeneo yao.


Akikagua usafi na ufungaji wa vifaa tiba katika Hospitali hiyo ya Mwabaruhi, alimwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, kuhakikisha uwekaji njia za watembea kwa mguu, ufungaji wa vitanda na vifaa muhimu unakamilika haraka ili kutoa huduma kwa wananchi mapema iwezekanavyo.

Vilevile, alimtaka kuhakikisha Kituo cha Afya Buzilasonga kinapata maji na kuondoa usumbufu kwa wananchi na watumishi kwa kukosa huduma hiyo.



Ukurasa 12

**Chonde chonde kope bandia, 'maskara' hazikuachi salama**



Ukurasa 13

Mamia watoto, vijana walivyosimama baada ya mkono wa kanisa kuwagusa



Ukurasa 14

**Dar High School ndani ya mikiki kuondoa pengo la elimu kijinsia**


Nipashe TESA

Jumanne Julai 23, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


SAYANSI

NA MAULID MMBAGA

# Ndivyo DIT ilivyomkomesha nzi wa matunda bila kiuatilifu sumu

NZI wa matunda na mboga wanaosababisha hasara hadi asilimia 80 ya mazao ni tishio kubwa la kilimo cha bustani nchini ambao kwa miaka mingi wamekwamisha uzalishaji, kwa kuharibu matunda yenye ngozi laini kama maembe.

Uharibifu huo ni hasara kwa wakulima wanaotegemea kupata chakula na kipato kwenye biashara ya mazao hayo.

Kwa mujibu wa wataalamu nzi hao hutaga mayai ndani ya matunda kama maembe, nyanya na matango ambayo hukomaa baada ya siku nane na kwamba nzi huyo anataga mayai hadi 1,500. Nzi hao huanguliwa ndani ya tunda na kuendelea kukua wakila tunda hilo na kusababisha kuoza na kubadilisha rangi ya ngozi katika kila hatua wanapokuwa na mwisho huoza.

Ili kuwadhibiti, kuwagundua na kuwafuatili wadudu hao, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imekuja na tiba. Mtafiti Mkiramweni Mbazingwa, anazungumza na Nipashe, akisema wadudu hao hasa spishi vamizi kama 'Bactrocera dorsalis' wanaharibu uzalishaji wa matunda na kuathiri biashara yake kimataifa.

Anasema ili kuwakabili wamebuni mbinu bora na sahihi zaidi za kuwagundua na kuwafuatilia ili kuwadhibiti kwa wakati na kwamba kupitia mradi wa Mtandao Unaobadilika wa Kufuatilia Mazingira Afrika Mashariki (AdEMNEA), wanatatua changamoto hiyo.

Anazungumzia ubunifu huo kuwa ni wa mtego unaendeshwa na nishati jua wenye kemikali ya 'pheromone' inayozalishwa DIT, inayowavuta wadudu karibu na dawa na kuwatumbukiza kwenye chupa au kontena na baada ya muda wanakufa.



Teknolojia ya kudhibiti inzi wa matunda. **PICHA: DIT**

Aidha, anasema mtego huo una injini inayowazungusha ili kuwamwaga inzi chini ya kontena ambao pamoja na kufa wanahifadhiwa kwa ajili ya hatua nyingine za kiutafiti.

Anaeleza kuwa mbali na pheromone mfumo huo hautumii dawa za kunyunyuzia wala kemikali hivyo kulinda mazingira na afya ya bayoanuai na kwamba wanafuatilia mara kwa mara idadi ya nzi wa matunda walionaswa na hivyo kupunguza kutembelea maeneo ulikotegwa na kuwakusanya kwa ajili ya uchambuzi wa taarifa zaidi.

Mbazingwa anasema kwa kutumia teknolojia hiyo mfumo wa ugunduzi wa kisasa unatoa taarifa sahihi na kwa wakati unaofaa ambazo zinafahamisha wakulima, maofisa wa kilimo na watafiti mambo mengi na kuwezesha kuandaa mikakati zaidi ya udhibiti.

Baadhi ya mikoa inayotumia teknolojia anasema ni Dar es Salaam na Pwani na imekuwa na manufaa na kwamba teknolojia hiyo inapatikana DIT na kila anayehitaji anaweza kuipata.

**FAIDA ZAKE**

Mbazingwa anaeleza kuwa mfumo huo una faida nyingi endapo mkulima atautumia, ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia ya kisasa kuwakamata wadudu waharibifu kwa kufunga mtego shambani kutayaacha mazao katika ubora halisi.

Faida nyingine ni kutoa data sahihi na ya wakati halisi, ambayo inaweza kuboresha mchakato wa kufanya maamuzi ya kudhibiti wadudu mbalimbali waharibifu.

Vile vile, anasema kupitia mfumo huo wakulima wanaweza kupokea taarifa za haraka kuhusu uvamizi wa wadudu hao shambani, hali itakayowezesha hatua za haraka za kupunguza athari zinazotokana na uharibifu wa wadudu husika.

Aidha, anaeleza kuwa maofisa wa kilimo wanaweza kutumia data zitakazotokana na mfumo huo, kufuatilia mielekeo ya wadudu na kupanga hatua za kanda nzima, huku watafiti wakiweza kuchanganua data iliyokusanywa ili kuchunguza aina za nzi wa matunda, tabia na kubuni mbinu bora zaidi za kudhibiti.

"Mitego iliyo na mifumo hiyo ya utambuzi wa hali ya juu sio tu inakamata nzi wa matunda bali pia hukusanya data muhimu. Kwa kutumia akili bandia (AI), na taarifa iliyokusanywa inaweza kutumika kutabiri milipuko ya wadudu ya siku zijazo na kuelewa athari zaidi za wadudu wa matunda katika uzalishaji wa kilimo.

"Mawazo kama haya ya utabiri ni muhimu kwa kutengeneza mikakati ya muda mrefu ya kudhibiti wadudu na kuhakikisha mbinu endelevu za kilimo zinapendekezwa na kutekelezwa kwa manufaa ya sekta hiyo na taifa kwa ujumla," anasema Mbazingwa.

**WASISITIZA TEKNOLOJIA**

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu, anasema wana mkakati wa kuratibu na kuhamasisha matumizi ya sayansi na teknolojia kupata majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikumba jamii hasa sekta ya kilimo.

"Iko haja kwa watafiti na wabunifu kuendelea kubuni teknolojia inayoweza kusaidia kuendeleza sekta ya kilimo, wanasayansi wanapofanya utafiti wao kikamilifu na matokeo kufika kwa wakulima, watalima kwa tija kwa kuinua maisha yao na uchumi wa taifa," anasema Dk. Nungu.

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

KUREMBA JICHO HATARI

# Chonde chonde kope bandia, 'maskara' hazikuachi salama

HUWEZI kuutenganisha urembo na mwanadamu japo wanawake zaidi, ndiyo maana hata mboni ya jicho ambayo ni kitu kinacholindwa zaidi kina vipodozi vyake.

Jicho nalo hurembwa likipakwa wanja kwenye nyusi, rangi mbalimbali kulizunguka bila kusahau kope bandika zinazobandikwa juu ya zile za asili, kisha ndani ya jicho hilo hurembwa kwa kutumia maskara.

Swali kwa wanaotumia, una uhakika gani kuwa maskara hiyo ni salama? Unapoichukua na kuitia jichoni, umewahi kuwaza kuwa imekwisha muda wa matumizi?

Ni dhahiri wengi hawafikiri hayo wala kuhusu tarehe za kuisha muda wa matumizi wa 'mekapu' hasa za machoni kuanzia maskara na kope bandia.

Vipodozi vya zamani vilivyokwisha muda vinaweza kuwa kiwanda cha kuzalisha vimelea na kuwa mwanzo wa maradhi ya macho, unaonya mtandao wa MMED.

Kama ambavyo kuna bidhaa nyingi feki kuanzia za kielektroniki, dawa za binadamu, mifugo na mimea, kadhalika kuna maskara feki ambazo si salama kwa afya ya macho.

Vipodozi feki vinaweza kusababisha kuwashwa machoni, uoni hafifu, maambukizo ya magonjwa machoni na mbaya kupata upofu.

Unaweza kuwa na hasara ya kudumu na zaidi ikiwa vigumu kutibu macho kama vipodozi hivyo vina viambato vya sumu, inaonya MMED.

Katika baadhi ya matukio hayo ya kutumia maskara zenye kemikali za sumu, mchakato wa kutibu na kuponya unaweza kuwa mgumu na wa gharama kubwa kuliko kumeza 'antibayotik' na kuweka dawa za matone ya macho, hivyo ni vyema macho.



### KUCHA BANDIA

Kwa upande wa rangi za kucha iwe kupaka na kubandika za bandia kuna wangapi wanachunguza iwapo muda wa matumizi umekwisha au zinatumika hadi lini?

Ni mambo ya kuangalia kutokana na sekta ya urembo kukua na wafanyabiashara wengi kuitumia kupata kipato kuanzia wanaopita mitaani kutoa huduma nyumba kwa nyumba na wengine wanaopatikana saluni.

Kubandika kucha bandia nalo ni jambo linayoshika kasi na kuchangamkiwa na wanawake wengi. Kumbuka unaweza kupata mzio au aleji, iwapo kemikali zinazotumiwa kupachika au kubandua kucha za bandia zinaweza kusababisha ngozi kuwasha na kuwa na vidonda, inasema MMED.

Unaweza kupata maambukizi kama usaha, uvimbe kwenye kucha. Maambukizi ya vimelea, kuvu na vijidudu vingine, yanaweza kugeuza kucha zako kuwa na rangi ya kijani.



Wakati mwingine kuwa na madoa meupe au njano, inasema MMED. Kucha dhaifu ni matokeo ya kuweka kucha bandia pia. Ili kuziondoa wakati mwingine unalazimika kuweka vidole vyako kwenye dawa ya 'asetoni' kwa dakika 10 au zaidi.

Kemikali hii inakausha sana kucha halisi na inaweza kuwasha ngozi. Baadhi ya kucha za bandia lazima zifunguliwe. Hiyo inaweza kufanya kucha zako za asili kuwa nyembamba, zinazovunjika haraka na dhaifu, hivyo yote hayo ni ya kuangali kulinda afya.

### KOPE BANDIA

Kwa mujibu wa BBC Swahili, zipo hatari kubwa za kiafya zinazotokana na kuweka kope bandia.

"Kope zetu za asili hufanya kazi muhimu, hulinda macho yetu kwa kuelekeza hewa mbali na mboni ya jicho, na kutufanya kupepesa, hatua ambayo pia huhakikisha kwamba macho yana majimaji vya kutosha." Inasema BBC.

Ukiwa saluni, kope bandia hushikanishwa na kila kope asili, moja kwa moja, zinaunganishwa na gundi ambayo inaweza kusababisha matatizo.

Wataalamu wengi wa vipodozi hufanya jaribio la awali la kuweka kope bandia kwenye eneo fulani la mwili, kwa kawaida kwenye mkono au nyuma ya sikio, ili kuangalia mizio au aleji za gundi, hata hivyo, hata ikiwa hakuna athari ya mzio, kemikali katika gundi inaweza kuwasha eneo la jicho na uzito wa gundi yenyewe inaweza kusababisha muwasho kwenye kope, inaeleza BBC.

Kwa mujibu wa utafiti, zaidi ya asilimia 60 ya wanawake waliripoti changamoto za maradhi ya jicho ya 'keratoconjunctivitis', hali ya jicho inayohusisha kuvimba kwa kornea na kiwambo kwa wakati mmoja, baada ya gundi ya kope bandia kugusa macho yao.

Inaongeza kuwa utafiti huo huo uligundua kuwa asilimia 40 ya wanawake walipata athari ya mzio kwa sababu ya gundi.

### GUNDI NA SARATANI

Kumekuwa na nyakati ambazo gundi ya kucha, ambayo ina nguvu zaidi imeuzwa kama gundi ya kope.

Katika mojawapo ya matukio ya kushtua ya kutumia kusikofaa, kope za mwanamke mmoja ziliachwa zikiwa zimeshikamana pamoja baada ya kuweka kope bandia kwa kutumia gundi kali.

Gundi ya kope inaweza kusababisha hatari kadhaa za afya, utafiti mmoja ulichanganua viambata 37 vya kibiashara na kitaalamu na kugundua uwapo wa 'formaldehyde', kemikali inayojulikana kusababisha saratani.

Uchambuzi huo uligundua kuwa asilimia 75 ya viambata 20 vya kitaalamu vilivyojaribiwa vilitoa formaldehyde, na gundi nne kati ya 17 za kibiashara pia zilikuwa na kemikali hiyo.

Anza kuwa makini usikimbilie kusaka urembo bila kujua usalama wake. Hasa mascara, kope za kubandika na rangi mbalimbali unazopaka kucha kwa sababu dunia ya sasa wapo wanaosaka fedha zaidi bila kujali hata kama itatokea wengine kupofuka.

## Ndivyo DIT ilivyomkomesha nzi wa matunda bila kiuatilifu sumu

INATOKA UK.11

### USHAURI WA WAKULIMA

Zakaria Charles, mkulima wa embe mkazi wa Mkuranga mkoani Pwani, anatoa wito kwa serikali kuwaunga mkono watafiti hao katika kuhakikisha kwamba suluhu wanazozitoa zinawafikia wakulima kwa wakati ili wapate tija ya kuwapo wataalamu hao.

Anasema anajihusisha na kilimo cha embe kwa zaidi ya miaka 10 sasa na changamoto kubwa inayowakabili ni uwepo wa wadudu hao wanaosababisha matunda kuoza yakiwa machanga na kwamba udhibiti wake bado haujawa wa uhakika.

"Mara nyingi tunatumia mbinu za kienyeji za kufukiza moshi kwa kuchoma majani chini ya mti ili kuwafukuza wadudu hawa lakini mbinu ya uhakika, hivyo ujio wa mfumo huo utakuwa na manufaa zaidi kwetu, nisisitize serikali kuwezesha upatikanaji kwa wingi wa mifumo hiyo ili itufikie kwa wakati," anasema Charles.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Mamia watoto, vijana walivyosimama baada ya mkono wa kanisa kuwagusa

WATOTO wanaoishi katika mazingira magumu wanapopata misaada na uangalizi bora wanajikwamua kimaisha na kuwa 'machapioni' wa mafanikio, si kwenye elimu pekee au ajira, bali pia huwa nuru na msaada kwa wengine ndani na nje ya familia.

Ni ushuhuda kutoka kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu wa mji mdogo wa Ilula ulioko Iringa, wanaoeleza jinsia walivyopata elimu na ujuzi wa aina mbalimbali na sasa wamebadili maisha yao na ya wengine.

Rebeca Muhema (20), anayetoka katika mji huo mdogo ni miongoni mwa wanaoufaika kupata misaada na elimu kuanzia msingi, sekondari hadi ufundi wa ushonaji kwenye Chuo cha Peace Maker mjini humo.

Anasema ni mapambano, ambayo yamempa ujuzi na ujira kwa kujiajiri akipambana na umaskini kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato tofauti na miaka ya nyuma.

Rebeca anawasilisha hali ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu ambao safari yao ilianza 2011 baada ya Shirika la 'Compassion International Tanzania la Arusha kuwatembelea mkoani Iringa na kuufikia mji mdogo wa Ilula kuangalia changamoto za wananchi ili kusaidia kuzitatua.

Baada ya utafiti iligundulika watoto wengi wa Ilula hawasomi, wametelekezwa na wazazi wao, wanaishi katika mazingira magumu, wamepata mimba utotoni na wengi wanaishi katika umasikini uliopindukia.

Mratibu wa Kituo cha Maendeleo ya Mtoto na Kijana cha Kanisa la Evangelist Assemblies of God Tanzania (EAGT) katika mji mdogo wa Ilula, Bujo Paight, anasema, ni mhusika katika safari ya kuwainua wanaoishi katika mazingira magumu.

Anazungumza na Nipashe akisema, baada ya kugundua matatizo Compassion, inatoa fedha kwa EAGT-Ilula kuwasaidia watoto kupata elimu ya msingi, sekondari hadi chuo kikuu.

"Tumesaidia watoto kwenye elimu, kiroho, kijamii na kiuchumi kwa msaada wa Compassion," anasema Paight na kuongeza kuwa kila mwezi shirika linatoa fedha kwa EAGT kuwahudumia watoto na vijana kufikia ndoto na malengo yao ya kiuchumi, kiroho na kiafya.



Mnufaika wa mafunzo ya ushonaji akiwa kazini. **PICHA: EAGT**

Anaongeza kuwa wanalipiwa ada ya shule, vifaa vya shule na michango mingine ili watoto wasome na kutimiza ndoto zao.

Lakini pia, wamejenga maktaba katika eneo la kanisa kwa ajili ya watoto kujisomea wakati wa muda wa ziada.

Anaeleza tangu 2011wamefunza watoto 401 ambao wamepata elimu kati yao 38 ni wa elimu ya awali, 75 ni wa shule ya msingi, 151 ni sekondari, wakati 16 ni vyuo vya kati, na wanne ni vyuo vikuu, 95 vya ufundi na wengine 22 hawajaanza shule wakiwa na miaka kati ya mmoja na miwili.

**KUFIKIA WAHITAJI**

Paight anasema kanisa linawapata watoto kupitia ushirikiano na serikali za mitaa na ofisi ya ustawi wa jamii na wanahakikisha watoto wote walio chini ya ufadhili wanahudhuria masomo.

Pia hivi sasa wametengeneza mkakati wa miaka mitatu wa kuongeza ufaulu wa watoto kutoka daraja la nne kuja daraja la pili na la kwanza na wana vijana ambao wamehitimu kutoka vyuo vya VETA na vikuu kutoka daraja la nne kuja la pili na la kwanza.

Anasema wanawasaidia vijana ambao wamehitimu sekondari, chuo kikuu, vyuo vya kati kama VETA kupata elimu ya ufundi na wakimaliza masomo wanapewa vitendea kazi kulingana na ujuzi waliousomea.

"Hadi sasa kuna vijana zaidi ya 40 ambao wamehitimu katika vyuo vya VETA, kati ya hao 10 wamepewa vitendea kazi kama vile kompyuta, ufundi rangi, kuchora, ujenzi, kushona, urembo na ususi wa bidhaa za aina mbalimbali, mapambo kwenye harusi, ufundi magari, umeme, uundaji na kushona viatu."

> Mbali na hilo, bado kuna zaidi ya vijana 78 wapo vyuoni wanaendelea na masomo ya ufundi.

"Mbali na hilo, bado kuna zaidi ya vijana 78 wapo vyuoni wanaendelea na masomo ya ufundi. Tunawapa elimu ya ufundi hata kama mtoto amefika chuo kikuu, lazima akasomee ujuzi ambao anaupenda ili wajiajiri kwa sababu tumeona kuna changamoto kubwa ya ajira, ujuzi watakaoupata utawawezesha kujiajiri," anasema Paight.

Lakini pia akimaliza huo ujuzi anawezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi vya ujuzi aliousomea.

**MAFANIKIO KIELIMU**

Katika vyuo vya kati wanafunzi watatu wamemaliza diploma ya uuguzi na ukunga, ufamasia na tayari wauguzi wawili wameajiriwa kwenye hospitali.

Mbali na hilo, vijana wawili wamehitimu diploma ya kozi ya maendeleo ya jamii kutoka Chuo cha Ruaha Community Development Training Institute na mmoja amehitimu Shahada ya Maendeleo ya Jamii kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mwaka huu, anaongeza Paight.

Watoto hao wanaishukuru Compassion kufanikisha mradi wa kusaidia wanaoishi katika mazingira magumu kwa sababu wamesoma na pia wamefundishwa ujasiriamali ili wakienda mtaani wajue pa kuanzia na wasikose cha kufanya.

Mbali na hilo mwaka 2016, kanisa la EAGT lilianza kufundisha wanafunzi elimu ya ujasiriamali, wakifundishwa kufuma na sasa wanafuma pochi za aina mbalimbali, mazulia, kutengeneza mapambo ya asili ya mikononi, shanga, chaki na pia kuuza bidhaa hizo kwa wateja wa ndani na nje ya Ilula.

Aidha, wamejifunza kutengeneza skafu, sabuni pamoja na vikapu vya asili vinavyotumia nyasi na kila Jumamosi walimu kutoka EAGT wanafundisha watoto kuhusu fani za kuchomelea, kufuma, kushona na kutengeneza bidhaa za ngozi hasa viatu vya shule.

Wahitaji hao wanasema wazazi wawasomeshe watoto bila ubaguzi, wapate elimu kama wa kiume ili waendelee kuzisaidia familia na mahali walipotoka.

ELIMU

NA ROMANA MALLYA

# Dar High School ndani ya mikiki kuondoa pengo la elimu kijinsia

## • Ina wanafunzi 400 wa sayansi

WASICHANA wasomi na wanaoweza kuwa sehemu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 hawawezi kupatikana kama hawatasoma na kuandaliwa kikamilifu.

Katika juhudi za kuondoa pengo la kijinsia la wasichana kuwa nyuma kielimu ikiwamo kuikimbia sayansi na teknolojia, serikali imechukua hatua za makusudi kwa kuwajengea shule mahususi katika mikoa 26 ya Bara.

Kwa Dar es Salaam, kazi imefanyika na sasa ipo Dar Girls High School iliyoko Kwembe wilayani Ubungo, iliyoanza masomo mwaka jana kwa kidato cha kwanza na cha tano pia.

Ujio wa shule hizo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, la kujenga taasisi hizo kila mkoa ili kuongeza wataalamu wanawake ambao ni wachache, pia kutimiza ndoto ya mtoto wa kike ambaye kila uchwao anakumbwa na madhila tofauti.

Madhila kama mimba na ndoa ututoni, kubakwa, kurubuniwa njiani wakati anapokwenda shuleni na kurejea nyumbani na kukatishwa masomo bila kuwapo sababu za msingi.

Jicho la Mama Samia likaona mbali zaidi na kuagiza ujenzi wa shule zenye uwezo wa kupokea wanafunzi 1,080 na kidato cha kwanza hadi cha sita.

Jumapili Julai 14, Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla na timu yake wanafika shuleni hapo, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya mkoa wa Dar es Salaam kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali.

Akiwa shuleni hapo, Makalla anaeleza historia kuanzia mwanzo hadi kukamilika kwa shule hiyo, akikumbusha namna mkandarasi wa kwanza alivyoikimbia. Anasema mkandarasi huyo alikimbia, akaletwa mwingine, aliyesema iwe hasara au faida atajenga na leo wasichana wanasoma.

Akawaeleza wanafunzi kuwa amepita hapo kuwasalimia kuona shule hiyo kubwa ya mfano mkoani Dar es Salaam.

"Zipo shule zenye historia Dar es Salaam mfano Sekondari za Zanaki, Jangwani na Forodhani, lakini hii kiboko yao. Hii ni jitihada za Rais Samia, ametoa fedha kila mkoa kujengwe shule kubwa ya mkoa."

"Sekondari hii ililetewa Sh. bilioni nne ijengwe hadi kukamilika. Ninaushukuru uongozi wa manispaa, meya na timu zenu kwa kuwa haikuwa kazi rahisi, ilifika wakati waliona wasukumane ili isimamiwe," anasema Makalla.



Ujumbe wa CCM ukiongozwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Mafunzo CCM, Amos Makalla, ukiwa Dar High School. **PICHA: ROMANA MALLYA**

### NENO KWA WANAFUNZI

Makalla kama mlezi wa mkoa, lakini pia mzazi, anawafunda wanafunzi hao kuwa shule hiyo haitokuwa na maana endapo hawataitumia kutimiza ndoto za Rais Samia za kujenga shule hizo ili kupata wataalamu wa sayansi wanawake.

"Ninajua hapa wapo mawaziri, wakuu wa mikoa, mabalozi, madaktari na walimu, tunataka watokane na shule hii, hataki kusikia utoro wala mimba.

"Basi ahadi hiyo kama ni ya kweli ninataka shule iwe na malezi mazuri ili mtoe watoto wenye sifa zinazofanana na Rais Samia," anasema akimwagiza mkuu wa shule hiyo pamoja na timu yake kutimiza lengo hilo.

Ofisa Elimu Sekondari, Voster Mgina, katika taarifa yake mbele ya Makalla, anasema kuwa halmashauri hiyo ina sekondari 74, kati ya hizo 36 ni za serikali na shule 38 zinaendeshwa na mashirika na watu binafsi.

Anasema Dar Girls High School ni moja ya shule nne ambazo zimejengwa kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) na kuongeza shule 36 na tatu za serikali za kidato cha tano na sita.

"Shule hii ilianza Agosti 2023, leo ina wanafunzi 460. Kidato cha kwanza wanafunzi 166, kidato cha tano 169 na kidato cha sita 135.Tuna wanafunzi 11 wenye mahitaji maalum." Anasema na kutaja idadi ya walimu kuwa ni 26 wanaotosheleza.

### GHARAMA ZA MRADI

Kuhusu gharama za ujenzi, Mgina anasema halmashauri imepokea Sh. bilioni 4.4 ambazo kati ya hizo, bilioni 1.3 zilitolewa katika awamu ya kwanza bilioni 1.1 awamu ya pili na Sh. milioni 350 zikatolewa kwenye umaliziaji.

"Awamu ya kwanza ya utekelezaji baada ya kupokea fedha, mradi umefikia asilimia 99 ambapo jengo kubwa lililobakia kumalizia ni la bwalo. Awamu ya pili umefikia asilimia 93," anasema.

Aidha, anasema katika Sh. bilioni 1.3 zilizotolewa na halmashauri zimetumika kutengeneza viti na meza takriban 700, vitanda 150, meza za bwalo 20 na viti 207.

### NISHATI SAFI

Mgina anasema halmashauri imesimika mfumo wa gesi ya kupikia shuleni hapo ambao umeanza kutumika na kwamba mtungi wa una kilo 1,000.

Itakumbukwa Rais Samia ni kinara wa agenda ya nishati safi ya kupikia inayolenga kuondokana na nishati chafu ya kuni ambayo kwa kiwango kikubwa inachangia uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti unaosababisha kuwapo kwa mabadiliko ya tabia nchi duniani.

Anasema halmashauri pia, imesambaza umeme, maji, kutengeneza mitaro na barabara za kiwango cha kokoto zenye urefu wa kilometa 1.4.

Kadhalika anasema wamejenga mifereji na njia za waenda kwa miguu za urefu wa kilometa 1.8.

Anasema mradi huo wa shule utakapokamilika utachukua wanafunzi wa kike 1,000 wa kidato cha kwanza hadi kidato cha sita wanaosoma sayansi.

Anasema utaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza, ili kufikia malengo yao na kuchangia wanasayansi wa kike kuongezeka nchini.

"Utafanikisha ulinzi wa watoto wa kike, kuwaepusha na mazingira hatarishi yanayowakabili hasa wanaosoma shule za kutwa kwa kuwa hawa wanakaa bweni.

"Utapunguza msongamano katika madarasa ambayo tayati yameshajengwa. Ni shule ya mfano Dar es Salaam. wengine wanaweza kujifunza," anasema.

### WANANCHI WAWAASA

Frank John, mkazi wa Mbezi, wilayani Ubungo anasema jitihada za serikali kuwekeza katika shule za mchepuo wa sayansi kwa mtoto wa kike utawanyanyua kielimu na nchi kupata wataalamu.

John anasema ujenzi wa shule za bweni ni moja ya mkakati wa kumlinda mtoto wa kile ambaye leo jamii inamchukulia ni mtu mzima na kumrubuni huku ikikatisha ndoto zake.

"Binti akielimika atajisimamia mwenyewe, akikosa elimu ataishia kudanganywa na mwisho wa siku anakuwa mama katika umri mdogo.

Rehema Masawe mkazi wa Ubungo, anasema Rais ana maono ya mbali hasa kwa kuzingatia dunia inahitaji wanasayansi wa kutosha ili kuja na majibu ya changamoto za sasa.

"Dunia inahitaji kuwa na wanasayansi wengi, tunaona nchi nyingine kila siku zimekuwa zikivumbua mambo mapya, kupitia shule kama hizi taifa litapata wataalamu wengi wabobezi katika nyanja tofauti.

"Ninampongeza Rais Samia kwa kuja shule hizi inawezekana leo jamii ambayo haijui umuhimu wa elimu, baada ya miaka kadhaa, watoto hawa wakawa walimu kwao kwa kuvumbua mambo mbalimbali ambayo ni changamoto kwao na kuyapatia ufumbuzi."

Anatoa ombi kwa serikali akitaka ieendelee kujenga shule hizi ikiwezekana kila wilaya iwe na shule hizo ili mtoto aliyeko pembezoni asiachwe nyuma.

Pia ziajiri walimu wenye utaalam ambao mtoto akimaliza kidato cha sita aweze kutafuta ufumbuzi wa changamoto zake binafsi na jamii inayomzunguka, anashauri. Kupitia mradi wa SEQUIP wa miaka mitano, serikali ilitenga Sh. trilioni 1.2 kwa ajili ya kujenga shule mpya za sekondari 1,026 kati ya hizo, shule 26 ni shule maalum za wasichana zinazojengwa kila mkoa shule moja.

Kupitia mradi wa kuboresha Elimu ya Sekondari kila mkoa umepewa bilioni nne kwa awamu mbili kujenga shule ya wasichana ya bweni, ambayo itakuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 1,080 na kidato cha kwanza hadi cha sita.





# COSTECH kuimarisha uhusiano Tanzania, Ghana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imepokea ujumbe wa Baraza la Ruzuku za Sayansi ( GCI) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kikazi na kuimarisha uhusiano baina ya Serikali ya Tanzania na Ghana.

Akipokea ujumbe huo, Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi (DCS), Immanuel Mgonja, alisema ziara hizo zinatoa hamasa kwa vijana kupenda masomo ya sayansi, ambayo ni suluhisho la kutatua changamoto ya ajira na kuliletea taifa maendeleo kijamii na kiuchumi.

Mratibu wa Baraza la Ruzuku la SGCI nchini Ghana, Wilfred Dennis, alisema wamejifunza COSTECH inavyosambaza taarifa kupitia studio zake.

"Tumejifunza utoaji vibali vya utafiti, upatikanaji wa huduma nafuu mtandao, usimamizi wa ajenda ya hakimiliki, ni tofauti na uendeshaji na MEIST inayotumia idara moja pekee," alisema na kuongeza kuwa: "Tutatekeleza mazuri tuliyojifunza tukirudi kwetu. Vilevile tunatazamia kushirikiana kuandaa ajenda za uombaji wa ruzuku."

Msimamizi Mkuu wa Fedha, Joana Amoako, alisema amevutiwa na idara ya fedha inavyosimamia upembuzi yakinifu kabla ya utoaji wa fedha za ruzuku kwa watafiti na wabunifu.

Kaimu Mkurugenzi wa MEIST Ghana, Nana Osei-Safo Wiafe, alisema amevutiwa na mfumo wa kulea wabunifu na watafiti.

"Ziara hii imenifanya niendelee kuyatekeleza mazuri ya kutoka hapa nchini kwangu," alisema Wiafe.

Meneja wa Sayansi Hai COSTECH, Dk. Paul Ochang'a, alieleza namna tume inavyosimamia fedha za ruzuku na uwasilishaji wa mada za mabazara ya SGCI yaliyofanyika Nairobi nchini Kenya mwaka jana na kuwa kivutio kwa watu wengi zaidi.

# Kanisa lazifariji kaya kwa msaada magodoro, malazi

**Na Paul Mabeja,** MANYONI

KANISA la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Rift Valley limetoa msaada wa mahindi, magodoro na mablanketi kwa kaya zaidi ya 160 baada ya nyumba na mazao kusombwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha Kijiji cha Sasajila wilayani hapo Mkoa wa Singida.

Askofu wa Kanisa hilo, John Lupaa, akikabidhi msaada huo kwa waathirika hao, alisema kuwa Januari mwaka huu kaya hizo zilikumbwa na mkasa huo uliosababishwa na mvua hizo za Elinino.

"Januari mwaka huu kaya hizi zilikumbwa na mafuriko yaliosababishwa na mvua kubwa za Elinino zilizo ambatana na upepo mkali wa kimbunga na kusababisha nyumba zao kubomoka na vyakula kusombwa na maji hali iliyowalazimu kulala katika jengo la kanisa kijijini hapa," alisema Askofu Lupaa.

Alisema kwa kushirikiana na uongozi wa serikali ya kijiji hicho, walibaini kaya zilizoathirika na mvua hizo na kuzipatia msaada huo ambao utawasaidia kwa kipindi kifupi.

Dk. Margareth Ndonde, Katibu na Mratibu wa Maendeleo ya Jamii wa Umoja wa Wanawake wa Anglikana Tanzania (UMAKI) Taifa, alisema msaada huo wametoa kwa kaya 167.

"Msaada huu wa mahindi, magodoro pamoja na mablanketi utakwenda kusaidia kaya hizi ambazo hivi sasa zinakabiliwa na changamoto ikiwamo ya kukosa makazi, chakula na malazi," alisema.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Weza B, Kijiji cha Sasajila wilayani hapa, Boniface Malecela, alilishukuru kanisa hilo kwa kutoa msaada huo kwa wakati mwafaka.

Malecela, alisema Januari mwaka huu kaya hizo zilikubwa na mkasa huo baada ya mvua zilizoambatana na kimbunga kubomoa nyumba zao, kuharibu vyakula na mafuriko kusomba baadhi ya vitu.

"Tangu wakati huo kaya hizi zimekuwa hazina makazi ya uhakika na chakula baada ya mashamba yao na akiba ya vyakula iliyokuwapo ndani kusombwa na maji. Maada huu uliotolewa leo utasaidia kupata ahueni angalau kwa miezi miwili wakati tukifanya maarifa mengine," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa msaada huo, Robert Daniel, alisema nyumba yake ilibomoka kwa kusombwa na mafuriko akiwa shambani.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Asia Messos, akizungumza jana na wakazi wa Kijiji cha Mwangeza na kuwahamasisha kushiriki katika zoezi la uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu. **PICHA:THOBIAS MWANAKATWE**

# Wahamasishwa kujiandikisha kupiga kura, uchaguzi wa mitaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Asia Messos, ametoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika zoezi la uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura na uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji utakaofanyika nchini baadaye mwaka huu.

Asia alitoa wito huo juzi wakati wa ziara ya kikazi ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Moses Machali ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wakazi wa Kijiji cha Mwangeza.

"Zoezi la uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura hapa kwetu litaanza Desemba 11 mpaka 17, 2024 tujitokeze kwa wingi hii ni haki ya msingi kwa kila mwananchi wa Mwangeza na Mkalama kwa ujumla, lakini tushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kuchagua viongozi sahihi," alisema.

Aliwakumbusha wajawazito kwenda kliniki mapema ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza wakati wa kujifungua watoto.

"Unapofika kliniki mapema wataalamu wetu wanakuwa katika nafasi nzuri ya kufanya uchunguzi mapema na kujua hali ya mama pamoja na mtoto. Nitoe wito kina baba tuwasindikize kina mama kliniki, kifo cha mama na mtoto kinaepukika," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, aliwataka wazazi kuungana kukomesha utoro wa wanafunzi wilayani hapa badala yake wawapeleke shule kwa maslahi mapana ya jamii na taifa.

Wakati huo huo; Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega, amezindua zahanati ya Igengu ikiwa ni mpango wa serikali wa kuhakikisha kila kijiji nchini kinakuwa na huduma za afya.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa zahanati hiyo, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha za kujenga kituo hicho na kuwataka wakazi wa kijiji hicho kulinda afya zao kwa kwenda kupata matibabu.

"Serikali imefanya kazi kubwa, Rais Dk. Samia kaleta zahanati na kaleta na umeme. Nampongeza pia mganga mkuu wetu, Dk. Solomon Michael kwa kazi kubwa anayofanya, niwapongeze pia wananchi. Niwasihi tulinde afya zetu, tuzingatie ushauri wa wataalamu wetu," alisema.





# Mama auawa, wanawe wakutwa wakiosha maiti, nguo alizovaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKAZI wa Mtaa wa Idundilanga Halmashauri ya Mji Njombe mkoani hapa, Tulivane Mkongwa (85), ameuawa kikatili kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani kwa kile kinachodaiwa ni imani za kishirikina.

Akizungumza na waandishi wa Habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, alisema kuwa bibi huyo aliuawa baada ya kuvamiwa nyumbani kwake majira ya asubuhi Julai 20, mwaka huu.

"Kuna kijana ambaye alikuwa anafanya kazi ya kuchunga ng'ombe kwa huyu bibi tangu siku ya tukio hajaonekana, kwa hiyo tunamtafuta kwa mahojiano maana ameishi na huyo bibi kwa muda mrefu, lakini ametoweka tu siku ya tukio," alisema Kamanda Banga.

Alisema pamoja na kumsaka kijana huyo, jeshi hilo linawashikilia watu wanne, wakiwamo watoto wawili wa marehemu huyo kwa mahojiano kuhusu tukio hilo.

"Hawa tunawashikilia kutokana na mazingira kwa sababu mtu ameuawa tukakuta wanafanya usafi wa nguo, mwili wa marehemu na eneo hilo ambalo alikuwa ameuawa," alisema Banga.

Alisema jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi kubaini sababu za watoto hao kushindwa kutoa taarifa za mauaji ya mama yao.

Ametoa wito kwa wananchi endapo wataona tukio la mtu kupoteza maisha wasiingilie wala kufanya chochote vinginevyo jeshi hilo litakosa ushahidi na mtuhumiwa halisi wa mauaji.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Idundilanga, Filoteus Mkongwa, alisema alipigiwa simu asubuhi kuwa mwananchi wake amepatwa na umauti, baada ya kufika mazingira waliyoyakuta ni tofauti kwani yanaonyesha alishambuliwa.

Mmoja wa majirani wa marehemu huyo, Magreth Mwenda, alisema taarifa ya tukio hilo alipata mara tu baada ya kurudi safarini akitokea jijini Dar es Salaam.

Alisema baada ya kutumiwa ujumbe alifika nyumbani hapo kwa mwanakikundi mwenzao ambaye ni mtoto wa marehemu huyo.

"Nikijua ni kifo cha kawaida, baada ya kuwauliza wanakikundi wenzangu wakaniambia ndani kuna polisi, huyu mama amepigwa na kitu kizito," alisema Mwenda..



Diwani wa Kata ya Utengule Usongwe, Yona Ntunjilwa (wa pili kushoto), akimkabidhi viatu mjane Enere Soso, mkazi wa Mtakuja Kivukoni, Mbalizi, Mbeya Vijijini. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali, akishuhudia tukio hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# M'kiti CCM aahidi kufunga taa sokoni

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, ameahidi kufunga taa maeneo ya soko la Ndanto la Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ili kuwawezesha wajasiriamali kufanya biashara usiku na mchana.

Vilevile Mwalunenge ameahidi kuwawezesha vijana 50 wa Kata ya Ndato kwa kuwapatia mbolea na mbegu ikiwa ni jitihada zake za kuwaunga mkono kuboresha kilimo cha viazi mviringo kwa msimu ujao na kuwainua kiuchumi.

Aliwataka vijana hao kuacha kujiingiza kwenye vurugu na badala yake waendelee kujikita kwenye shughuli zao za kiuchumi ili kujiletea maendeleo na kuvutia wawekezaji.

"Tujitahidi kudumisha amani ili eneo letu liendelee na sifa nzuri, ndio maana nimeamua sasa kuwawezesha vijana 50 kupata mbolea na mbegu ili mlime kwa wingi na kukuza kipato chenu," alisema Mwalunenge.

Aliahidi kuwaunga mkono wananchi kwenye ujenzi wa kituo cha Polisi cha kata hiyo ili kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo.

Baadhi ya wa kata hiyo waliiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya barabara ili kuwarahisishia usafirishaji wa mazao ya kilimo na biashara.

Juhudi Mwambenja, alisema wakati wa masika wanashindwa kusafirisha viazi kutoka shambani kwenda sokoni na mbolea kwenda shambani hali ambayo inazorotesha uzalishaji.

Alisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kusafirisha mazao kutoka shambani kwenda barabarani kwa kukodi vibarua.

# Mgogoro wa mpaka Mbarali, Makete pasua kichwa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WATAALAMU wa ardhi wa mikoa ya Mbeya na Njombe wameagizwa kuainisha upya mpaka kati ya Makete na Mbarali ili kutatua mgogoro katika baadhi ya maeneo ya wilaya hizo.

Agizo hilo lilitolewa wakati wa kikao cha Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa hiyo kilichofanyika Kijiji cha Kimani kujadili mgogoro huo ambao umekuwa chanzo cha wananchi kukosa baadhi ya huduma muhimu.

Inadaiwa kuwa kutokana na mgogoro huo, wakazi wa kijiji hicho cha Kimani hawakuhesabiwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 na hakina anuani ya makazi kama ilivyo kwa vijiji vingine vya mikoa hiyo na nchini.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Maono Sanga, alisema mgogoro huo unaviathiri vijiji saba vya Ruaha, Mfumbi, Ikovo na Kimani kwa upande wa Makete na Mwaluma, Kibaoni na Mtamba kwa Mbarali.

Alisema mipaka ya vijiji hivyo haieleweki hali ambayo inasababisha baadhi ya wananchi kutotambua wilaya sahihi za kuwajibika na kupata huduma za jamii.

"Kijiji cha Kimani ndio kabisa hakieleweki maana hakina anuani ya makazi, tumepambana kuandaa mihutasari lakini mpaka sasa hatujapata suluhisho, unaweza ukakuta nyumba ziko eneo moja lakini wapo wanaowajibika Makete na wengine Mbarali," alisema Sanga.

Patrick Kyando, Mkazi wa Kijiji cha Kimani, alisema mgogoro wao sio wa kupigana bali ni wa maneno na kuonya kuwa usipotatuliwa unaweza kusababisha madhara zaidi.

Alisema vijiji ambavyo vipo kwenye mgogoro huo havipati baadhi ya huduma kutokana na mgogoro huo na kuiomba serikali kuingilia kati ili kupata ufumbuzi.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema mgogoro huo huenda unachochewa na baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwa wakiwaaminisha wananchi wakiwachagua mgogoro utakwisha.

Alisema wataalamu hao watashirikiana na kamati za ulinzi na usalama za wilaya zote mbili na wananchi kumaliza mgogoro huo.

"Mipaka iliyopo ni ya wakoloni, lakini pia kuna mipaka mipya ambayo tumeianzisha wenyewe, zamani Mkoa wa Mbeya ulikuwa unapakana na Iringa kabla ya kuzaliwa Mkoa wa Njombe, hata Wilaya ya Mbalali zamani ilikuwa sehemu ya Wilaya ya Mbeya, kwa hiyo tunataka tuumalize mgogoro huu kwa kuainisha upya mipaka," alisema Mtaka.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wakazi wa maeneo ya mgogoro huo kuendelea na shughuli zao kwa amani wakati serikali ikijiandaa kutatua.

Alisema mgogoro huo lazima utatuliwe kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu kwa kuwashirikisha viongozi wa pande hizo mbili.

Mbarali ni miongoni mwa wilaya ambazo zinakabiliwa na migogoro ya ardhi ikiwamo wa wakazi wake na hifadhi za taifa, wakulima na wafugaji, wakulima wadogo na wawekezaji.



# Watendaji wakuu wa serikali wapigwa msasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said, amewataka wakuu wa taasisi za serikali kuandaa mikakati ya serikali kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

Zena alitoa rai hiyo jana wakati akifungua semina kwa watendaji wakuu wa serikali, wakiwamo makatibu wakuu, manaibu wao na wakurugenzi iliyoandaliwa na taasisi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya serikali.

Alisema lazima watumishi wafahamu mikakati ya taasisi na serikali  na kutoa michango yao ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Alisema changamoto ya ufinyu wa fedha unapelekea mikakati mingi kukwama na kwamba lazima kuwa na mipango, nyenzo na rasilimali watu katika kutekeleza hilo.

Zena alisema kutokuwapo mawasiliano kunachangia kukwama  kwa mikakati kutokana na kukosekana kwa taarifa kwa watendaji na kuwataka washiriki hao kuhakikisha mafunzo hayo yanaleta tija.

“Baada ya mafunzo haya ya siku mbili kila mtu atajitathmini wapi alikuwa anakosea na kufanikisha malengo ya taasisi zetu ili maisha ya Zanzibar kuwa bora,” alisema Zena.

Washiriki wa mafunzo hayo, waliahidi kubadilika katika utendaji wa kazi zao ili kuleta tija kwa taifa.

**Alisema lazima watumishi wafahamu mikakati ya taasisi na serikali na kutoa michango yao ili kufikia malengo yaliyowekwa.**

# Wabunge Marekani waahidi makubwa wanawake, vijana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WABUNGE wa Bunge la Congress la Marekani wasema wameridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na serikali na asasi za kiraia kuimarisha uchumi wa wanawake nchini.

Akizungumza katika Maonesho ya Kilimo Dole Kizimbani Unguja mwishoni mwa wiki iliyopita, kiongozi wa ujumbe wa wabunge hao, Katerine Klark, alisema Serikali ya Marekani itaendelea kutoa misaada nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata manufaa.

Katerine ambaye ni Mnadhimu wa Chama cha Democratic katika bunge hilo, alisema misaada ya nchi hiyo inayotolewa kupitia Shirika la Misaada Kimataifa la Marekani (USAID) kwa vijana na wanawake itaimarishwa ili kuleta maendeleo zaidi kwa makundi hayo.

“Marekani imekuwa mshirika wa maendeleo ya Tanzania na kimsingi tumeridhika na matokeo ya misaada inayotolewa kwani tumeshuhudia wanawake na vijana ambao kila siku wanafanya mambo mengi kujinufaisha na kunufaisha nchi na watu wake,” alisema.

Akizungumzia changamoto za mabadiliko ya tabia nchi zilizotajwa kuathiri sekta ya kilimo hasa wa zao la mwani, alisema Marekani itaendelea kutafuta suluhu na kuwapongeza wanawake wa Zanzibar kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi.

“Kupitia Mradi wa Feed the Future tumeshuhudia kina mama na vijana wakijihusisha na shughuli za uzalishaji kwenye kilimo cha mazao ya mboga mboga kinachotumia teknolojia ya kisasa bila ya mbolea za kemikali,” alisema Katerine.

Mbunge wa Ohio 14 nchini humo, David Joyce ambaye ni mjumbe wa kamati ya matumizi ya bunge hilo, aliwahakikishia wajasiriamai hao kuwa wataendelea kuwapatia msaada wakulima na wanawake ili kupata rasilimali zaidi  za usaidizi wa kitaalamu kupitia kilimo na uchumi wa buluu.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Mwanahamis Ramadhani Hassani, alisema kabla alikuwa analima kilimo cha hasara kutokana na mbolea zenye kemikali na kupoteza mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 50.

**Mbunge wa Ohio 14 nchini humo, David Joyce ambaye ni mjumbe wa kamati ya matumizi ya bunge hilo, aliwahakikishia wajasiriamai hao kuwa wataendelea kuwapatia msaada wakulima na wanawake ili kupata rasilimali zaidi za usaidizi wa kitaalamu kupitia kilimo na uchumi wa buluu.**



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, akizungumza katika mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yataka uhuru wananchi kuchagua viongozi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT Wazaendo, Othman Masoud Othman amesema wananchi wanapaswa kupewa uhuru wa kidemokrasia wa kuchagua viongozi wa kuwaongoza katika uchaguzi mkuu ujao.

Othman aliyasema hayo wakati akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Uwanja wa Mwenge uliopo Jimbo la Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema nchi ni mali ya wananchi na ndio wanapaswa kuamua nani wa kuwaongoza kupitia utaratibu wa kidemokrasia bila ya kuwapo mizengwe ya aina yoyote kwa kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

“Hii nchi ni Wazanzibari na wao ndio waamue wanataka nani awaongoze, ukimpenda wewe usimpende wewe haikuhusu hii ni nchi yao,” alisema Othman.

Alisema Zanzibar bado inahitaji kuwa na mamlaka kamili, ikiwamo ushuru wa forodha, huduma za posta na mawasiliano, sarafu, fedha na huduma za bandari.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema kilomita 257 za barabara zinazojengwa Zanzibar zitakuwa hazifai baada ya miaka saba kutokana na kutumika aina ya lami baridi ambayo teknolojia yake haifai kutokana na mazingira visiwani hapa.

Ladhu, alisema Wazanzibari wanapaswa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kufanikisha mkopo wa ujenzi wa miundombinu kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Uingereza.

Alizitaja barabara zilizopaswa kunufaika kutokana na mradi huo kuwa ni Mkoani/Chakechake, Uwanja wa Ndege Pemba, Kisauni/Fumba na Tunguu/Makunduchi.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio ya mradi huo bado unaendelea kusuasua wakati ujenzi wake ulitarajia kuanza Novemba mwaka jana.

Alisema ujenzi wa barabara hizo unatakiwa kusimamiwa kwa umakini kwa manufaa na maendeleo ya Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**PETER JOSEPHAT BALLY** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE273257** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji DAR ES SALAAM mnamo terehe 08/01/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/150354/2024.**

## KUPOTEA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**ASSAD HASHIM JUMA** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki kiwanja namba **37 Kitalu "KK" (HD)** kilichopo Mhumbu Manispaa ya Shinyanga kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SHI/SHI/4343/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IMANI ALFRED BASYAGILE** anatangaza kupotea Kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 135 BVZ.** aina ya Toyota OPA, Chassis No. **ACT100002507.** Engine No. **1AZA482047.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/30319/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAXMILLIAN WILLIAM MALLYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 496 BVM – DAIHATSU HIJET TRUCK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/150961/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASWA**
**Kituo cha NYALIKUNGU Mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Ndoa Na. 24/2024**

**Jina la mdai: MALELEMBA SALUMU MAHEMELA**

**Jina la mdaiwa: MAGRETH SAMWEL MAHONA**

**KUITWA SHAURINI**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: MAGRETH SAMWEL MAHONA WA KIDAGANDA**
**K.K MWENYEKITI WA KITONGOJI CHA KIDAGANDA**
**K.K AFISA MTENDAJI KIJIJI WA KIDAGANDA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
**ANADAI TALAKA**
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 mwezi wa 07 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17 Mwezi 07 Mwaka 2024.

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA — HAKIMU — HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 7026/2024**

**ELIZABETH MESOMAPYA................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MABWAYI MSENZI.......................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: MABWAYI MSENZI**

**POPOTE PALE ULIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 7026/2024**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya **Mhe. Jaji I. D. MUSOKWA,** wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu kamili (9:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 13/08/2024.
**HIVYO BASI;** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** hutofika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 Mwezi wa Julai, 2024

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION No 12982 OF 2024**

**In the matter of the estate of the late JOB NYANGUSI MULIMBA of Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for Letters of administration by JONATHANI GIDION MAKALI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 7...................... 2024

**Dated at Dodoma this 6 day of 6................2024**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1068/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SIWAZURI AMIRI SAIDI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA SUNDAY HASSAN OMARY**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 mwezi 07 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Limetokewa leo tarehe 22 mwezi 07 mwaka 2024.

mwezi 07 mwaka 2024
HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.28/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SWALEHE ALLY LAHE wa CHINANGALI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA TATU SALUMU SELEMANI**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06 Mwezi 08 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 19 Mwezi 07 Mwaka 2024.

HAKIMU

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Makazi ya Bobi Wine yazingirwa Uganda

**KAMPALA,** Uganda

MWANASIASA mkuu wa upinzani nchini Uganda Bobi Wine amesema maofisa wa usalama wamezingira makao makuu ya chama chake, ikielezwa kuwa hatua hiyo inakuja kuelekea maandamano yaliyopangwa kufanyika leo kupinga kile wanaharakati wanasema ni kukithiri kwa ufisadi.

Wine, ambaye jina lake halisi ni Robert Kyagulanyi, aliwaambia waandishi wa habari jana kwamba makao makuu ya Chama chake cha National Unity Platform (NUP) katika eneo la Kavule, nje na mji mkuu wa Kampala yalikuwa yamezingirwa.

Ripoti ya maofisa wa usalama kuzingira makao makuu ya chama chake Bobi Wine imekuja pia ikiwa imepita siku mbili tangu Rais Yoweri Museveni, kuwaonya wanaopanga kuandamana kwamba wanacheza na moto.

Mamlaka nchini Uganda imekuwa ikikabiliana vikali na Chama cha NUP kinachoongozwa na mwanamuziki wa zamani ambaye alishindwa na Rais Museveni katika uchaguzi wa 2021.

Pia ilielezwa kuwa siku chche zilizopita polisi nchini Uganda walidai kutoa taarifa kwa waandaaji wa maandamano hayo kwamba hawajapewa kibali cha kuendelea na mipango yao ya Jumanne.

Maandamano hayo yameitishwa na vijana katika taifa hilo la Afrika Mashariki chini ya kauli mbiu maliza ufisadi.

Vijana nchini humo wameonekana kuiga mfano wa wenzao kutoka nchini Kenya maarufu kama Gen Z wanaoandamana kushinikiza mageuzi katika serikali ya Rais William Ruto.

Mapema mwaka huu, Marekani na Uingereza zilitangaza vikwazo dhidi ya baadhi ya maofisa katika serikali ya Uganda akiwamo spika wa bunge kwa madai ya kuhusika na ufisadi. **RFI**






Rais Joe Biden akiwa ameinua mkono wa Makamu wa Rais, Kamala Harris, aliyempendekeza kuwa mteule wa Chama cha Democratic katika kinyang'anyiro cha urais. **PICHA: MTANDAO**

# Mjue Kamala anayejiandaa kuvaa viatu vya Mzee Biden

**NEW YORK,** Marekani

BAADA ya Rais wa Marekani Joe Biden kuchukua uamuzi wa kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kugombea urais na kumpendekeza makamu wake Kamala Harris kuchukua nafasi hiyo, Donald Trump ameibuka na kusema kwamba ni rahisi kumshinda.

Rais Biden alithibitisha juzi kwamba hatagombea tena katika uchaguzi wa urais unaotegemewa kufanyika Novemba mwaka huu, baada ya shinikizo kuzidi ndani ya chama chake cha Democratic kwamba ajiondoe katika nafasi hiyo, hali iliyomsukuma kumpendekeza Kamala mwenye umri wa miaka 59.

Trump mwenye umri wa miaka 78 alisema Rais Biden hakupaswa kugombea muhula wa pili, huku akihoji uwezo wa kiongozi huyo kusalia madarakani kwa muda uliobakiwa muhula wake.

"Joe Biden hakufaa kugombea urais, na kwa hakika hafai kuhudumu na hakuwahi kamwe! ... Tutateseka sana kwa sababu ya urais wake, lakini tutarekebisha uharibifu ambao amefanya haraka sana," Trump aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa Truth Social.

Katika chapisho alilolitoa kupitia mtandao wa kijamii Rais Biden alisema imekuwa heshima kubwa maishani mwake kuhudumu kama rais wa Wamarekani, huku akitoa wito kwa wananchi kumuunga mkono Makamu wake Kamala aweze kupeperusha bendera ya chama chao kwa nafasi ya urais.

"Na ingawa imekuwa nia yangu ya kutaka kuchaguliwa tena, naamini ni kwa manufaa ya chama changu na nchi yangu mimi kukaa pembeni," alisema.

Rais Biden mwenye umri wa miaka 81 amekuwa akikabiliwa na wito wa kusitisha kampeni tangu mdahalo dhidi ya Donald Trump wiki tatu zilizopita, ambako alionekana kuwa dhaifu, akipambana kueleweka.

Wakati akithibitisha kuwa hatashindana na Trump katika uchaguzi wa Novemba, Biden ameashiria kuwa atasalia kama rais hadi mwisho wa muhula wake.

Baada ya kuthibitisha kuwa anajiondoa katika kinyang'anyiro cha urais, Biden alimwidhinisha Makamu wa Rais, Kamala Harris kuchukua nafasi yake. Akisema kumchagua Harris ulikuwa uamuzi bora zaidi ambao aliufanya.

"Leo nataka kumuunga mkono kikamilifu na kumwidhinisha Kamala kuwa mteule wa chama chetu mwaka huu. Wanademokrati ni wakati wa kuja pamoja na kumshinda Trump, hebu tufanye hivi," alisema Biden.

Harris alijitosa katika siasa baada ya kupanda vyeo na kuwa mwendesha mashtaka mkuu wa California. Wakati wake katika Ikulu ya White House, na kwamba hakufanya mengi kuinua wasifu wake wa umma.

Ilielezwa kuwa alionekana kuwa katika kivuli cha Biden na kushambuliwa na Chama cha Republican kuhusiana na juhudi zake za kuzuia mmiminiko wa wahamiaji wanaowasili kutoka Mexico.

Aidha, ilielezwa kuwa Harris, ana faida zaidi ya wagombeaji wengine wanaowezekana kwa sababu ya uwezo wake wa kuzitumia fedha za kampeni ambazo tayari amechangisha na Biden.

Kampeni hiyo hivi karibuni iliripoti kuwa na kiasi cha dola milioni 91, huku kamati za kampeni za washirika zikifanya kiwango jumla kuwa zaidi ya dola milioni 240.

Kiongozi wa wengi katika Baraza la Seneti Chuck Schumer ametoa pongezi kwa Rais Biden baada ya uamuzi wake wa kutowania muhula wa pili katika uchaguzi wa rais wa Novemba.

"Rais Biden amekuwa sio tu rais mzuri na kiongozi mzuri wa sheria, lakini ni binadamu wa ajabu sana," Schumer alisema.

Mdemokrati huyo alisema uamuzi wa Biden "haukuwa rahisi, lakini aliweka tena nchi yake, chama chake, na mustakabali wetu mbele. Joe, leo inaonyesha wewe ni mzalendo wa kweli na Mmarekani halisi."

Pamoja na wabunge wengine kadhaa wa Democratic, Schumer alimwambia Biden kwa faragha kuwa itakuwa bora kwa nchi na Chama cha Democratic ikiwa atahitimisha kampeni yake ya kuchaguliwa tena.

**KAMALA NI NANI**

Inaelezwa kuwa miaka mitano iliyopita, Kamala alikuwa seneta katika Jimbo la California akitarajia kushinda uteuzi wa Chama cha Democratic kuwa rais.

Alianza kazi yake katika Ofisi ya Mwanasheria wa Wilaya ya Alameda na kuwa wakili wa wilaya, na mwaka 2003 alikuwa mwendesha mashtaka mkuu wa San Francisco.

Ilielezwa kuwa kabla ya kuchaguliwa kuwa mwanamke wa kwanza mweusi kuhudumu kama mwanasheria mkuu wa California, wakili mkuu na ofisa wa utekelezaji wa sheria katika jimbo lenye watu wengi zaidi la nchini Marekani.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa alipata sifa kama mmoja wa nyota wanaochipukia wa Chama cha Democratic, akitumia kasi hiyo kumsukuma kuchaguliwa kama seneta mdogo wa California Marekani mwaka 2017. Vile vile, ilielezwa kuwa malengo yake ya urais hayakufaulu 2020, ikielezwa kuwa utendaji wake mahiri wa mijadala haukutosha kufidia sera zilizotamkwa.

Ilielezwa kuwa kampeni yake ilikufa katika kipindi cha chini ya mwaka mmoja na ni Rais Biden ambaye alimrejesha Kamala kwenye darubini ya kitaifa kwa kumweka kwenye tiketi yake.

Katika hatua nyingine, Machi 2023 Kamala alipotembelea Tanzania alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kama bingwa wa kuimarisha demokrasia. **DW/BBC**

# NGAO YA JAMII HAKUTAKUWA NA DAKIKA 120 - BODI YA LIGI

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imebainisha kuwa hakutokuwa na dakika za nyongeza kwa michezo yote itakayopigwa kwenye Ngao ya Jamii inayotarajiwa kuanza kupigwa Agosti 8, mwaka huu.

**Ofisa Habari wa Bodi hiyo, Karim Boimanda, amesema mechi zote zitachezwa kwa dakika 90 na baada ya hapo ni mikwaju ya penalti itaamua mshindi.**

Boimanda alisema hayo, alipokuwa akibainisha baadhi ya kanuni zitakazotumika kwenye michuano hiyo, pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza Agosti 16, mwaka huu.

Mbali na hayo, amesema wachezaji watakaotumika kwenye mechi hizo ni wale tu ambayo watakuwa wamekamilisha usajili wa kucheza Ligi Kuu na si vinginevyo kwani huko nyuma imeshawahi kutokea timu moja kuchezesha kwenye Ngao ya Jamii mchezaji ambaye baadaye ilibainika bado alikuwa hajakamilisha taratibu za kucheza ligi.

"Wachezaji wanaoruhusiwa kucheza Ngao ya Jamii ni wale ambao usajili wao umekamilika tu, ambao wameshasajiliwa kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa na hakutokuwa na dakika za nyongeza kwa mechi zote, kuanzia za nusu fainali, fainali hadi kusaka mshindi wa tatu, zikiisha dakika 90, zitapigiana mikwaju ya penalti," alisema Ofisa Habari huyo.

Agosti 13, 2022, Fiston Mayele alifunga mabao yote mawili, Yanga ikiichapa Simba 2-1 katika mechi ya Ngao ya Jamii, lakini baadaye iligundulika alikuwa hajakamilisha usajili kitu kilichosababisha kutocheza mechi za awali za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huo.

Aliitaja kanuni nyingine ni kwamba, mchezaji yeyote ambaye alimaliza Ligi Kuu msimu uliopita akiwa na kadi nyekundu au adhabu ya kusimamishwa hata mechi moja kwa kuwa na kadi tatu za njano na hakuzitumikia kwa sababu ligi ilikuwa imemalizika, hatoruhusiwa kucheza kwani atatakiwa kutumikia adhabu yake.

"Kanuni hizi zinatumika pia kwenye Ligi Kuu. Kwa hiyo hata adhabu zinaingiliana, mchezaji mwenye kadi na hakutumikia hatatusubiri mpaka ligi hivyo atazitumikia kwenye Ngao ya Jamii. Lakini yeyote ambaye atapata kadi nyekundu kwenye michezo hiyo, ataitumikia pia kwenye michezo ya ligi," alisema.

Alisema wameamua kuanika baadhi ya kanuni hizo kutokana na mashabiki wengi kuwa na mkanganyiko hasa inapokuwa michezo kama hiyo ambayo ni ya mtoano, wasijue nini kinafuata baada ya timu kutoka suluhu.

Agosti 8, saa 10:00 jioni, Azam itakipiga dhidi ya Coastal Union, Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar. Na saa 1:00 usiku Simba itavaana na Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam na fainali ya Ngao ya Jamii itapigwa hapohapo Agosti 11, mwaka huu.

## *Karihe atimkia Mashujaa FC*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Mtibwa Sugar, Seif Karihe amejiunga na Mashujaa FC ambapo atakuwa sehemu ya kikosi kwa msimu ujao wa Ligi Kuu baada ya timu yake kushuka daraja.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa, mchezaji huyo anakwenda kuziba pengo lililoachwa na Adam Adam ambaye ametimkia Azam FC.

"Rasmi sasa Karihe ni mchezaji wa Mashujaa FC, na tuna matumaini ataitumikia timu yetu kwa bidii kama ambavyo alikuwa anafanya kwenye timu alizochezea," ilieleza taarifa rasmi ya klabu hiyo.

Mbali na kuondokewa na Adam, Mashujaa pia ilimpoteza mmoja wa mastraika wake tegemeo aliyechangia kwa kiasi kikubwa isishuke daraja wala kwenda 'paly off' kwa mabao aliyofunga katika mechi kadhaa za kuelekea kumalizika kwa ligi. Reliants Lusajo ambaye amekwenda kujiunga na Dodoma Jiji FC, pamoja na kiungo mshambuliaji, winga na wakati mwingine akicheza kama straika, Omari Omari, aliyetimkia Simba.

Karihe, ambaye amezichezea klabu mbalimbali nchini kama vile Mafunzo ya Zanzibar, Ruvu Shooting, Azam FC, Lipuli FC, Mbeya City na Dodoma Jiji kabla ya kutimkia Mtibwa Sugar anakuwa mchezaji wa tisa kujiunga na kikosi hicho kwa msimu ujao wa ligi.

Wachezaji wengine ni Abdulmalick Zacharia kutoka Namungo, straika wa zamani wa Simba, Mohamed Mussa, kiungo Mathew Michael (Mbeya City) na Carlos Protas ambaye ni beki wa kati kutoka Biashara United.

Wengine ni straika, Ismail Mgunda kutoka Singida Black Stars, Robert Mathias Makidala na golikipa, Yusuph Dunia (wote KenGold) na Ally Nassor 'Ufudu' akitokea Kagera Sugar.



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini Ismailia, nchini Misri juzi kujiandaa na msimu mpya wa mashindano 2024/25. **PICHA: SIMBA**

# Tekeleza FC kutekeleza lengo lao Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kwamba ndiyo kwanza inakwenda kuonja mikikimikiki ya Ligi Kuu Zanzibar, timu ya Tekeleza FC imetangaza mapema nia ya kutekeleza lengo lao la kuutaka ubingwa wa ligi hiyo kuelekea msimu mpya wa 2024/2025.

Timu hiyo kwa mara ya kwanza imepanda daraja kutokea Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba na itacheza Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Wahidi Mbarouk, alisema ameshazisoma mbinu za timu zote za Ligi Kuu Zanzibar hivyo itakuwa rahisi kwao kufanya vizuri katika michezo ya ligi hiyo katika mbio za kuwania ubingwa.

Alisema kitu kikubwa alichokifanyia kazi ni timu zinazopanda daraja kushindwa kusalia Ligi Kuu kwa kucheza msimu mmoja na kushuka Daraja la Kwanza jambo ambalo kwa upande wa timu yake ameahidi halitojitokeza.

Alisema katika kuhakikisha anatimiza malengo ya timu atafanya usajili mkubwa ambao utakuwa na kikosi imara na kipana kitakachoweza kuhimili mikikimikiki ya Ligi Kuu Zanzibar.

Mbarouk alisema mpango wao mkubwa ni kusajili wachezaji wenye uzoefu mkubwa wa Ligi Kuu ambao wataisaidia timu yao kufanya vizuri katika msimu wa kwanza wa ligi hiyo ngumu.

"Tunaanza msimu wetu wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar na lengo letu kubwa ni kuchukua ubingwa na tunauwezo wa kutimiza lengo letu kutokana na usajili tutakaoufanya," alisema.

Aidha, alisema anajua ugumu uliopo katika ligi hiyo, na hiyo imetokana na timu kongwe kufanya maandalizi ya nguvu.

Hata hivyo, alisema timu hiyo inatarajia kuanza mazoezi yake ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu mwishoni mwa mwezi huu.

**Tunaanza msimu wetu wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar na lengo letu kubwa ni kuchukua ubingwa na tunauwezo wa kutimiza lengo letu kutokana na usajili tutakaoufanya.**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### CALAFIORI AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kufikia makubaliano ya thamani ya pauni milioni 42.1 na Bologna kwa beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Sports)***

#### TOMORI ATAKIWA MILAN

KLABU ya West Ham ina nia ya kutaka kumnunua beki wa AC Milan mwenye umri wa miaka 26, Fikayo Tomori. ***(Mail)***

#### CASH KUPELEKWA SOKONI

KLABU ya Aston Villa iko tayari kumuuza beki wa kulia wa Poland, Matty Cash mwenye umri wa miaka 26, msimu huu mpya. ***(Football Insider)***

#### LIGT ATAKIWA KUONDOKA

RAIS wa heshima wa Klabu ya Bayern Munich, Uli Hoeness amependekeza beki Mholanzi Matthijs De Ligt mwenye umri wa miaka 24, ambaye anasakwa na Manchester United kuondoka katika klabu hiyo msimu huu. ***(Sky Germany)***

#### BRUYNE, WASAUDIA BADO

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ubelgiji, Kelvin de Bruyne mwenye umri wa miaka 33, hajaafikiana makubaliano na Klabu ya Saudi Arabia, Al Ittihad licha ya kuwapo kwa ripoti. (Sportsport)

#### AMRABAT NA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imeamua kutoanzisha chaguo la kumsajili kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27, kwa mkataba wa kudumu. ***(Tuttomercato)***

#### DIABY HUYOOO SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Aston Villa, Mfaransa Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 25, anatarajiwa kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Al Ittihad wiki ijayo. ***(Sportsport)***

#### MCTOMINAY HAONDOKI UTD

MANCHESTER United haitaki kumruhusu kiungo wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27 kuondoka Old Trafford, huku Fulham na Tottenham Hotspur zikimnyatia. ***(Standard)***

#### FELIX AWANIWA VILLA

ASTON Villa wanataka kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 24. ***(Sun)***


#### SKIPP KURUHUSIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumruhusu Oliver Skipp mwenye umri wa miaka 23, kuondoka katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

#### GOMEZ AWINDWA

KLABU ya Brighton imefanya mazungumzo na Inter Miami kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Paraguay, Diego Gomez, 21. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ØDEGAARD, JESUS NDANI ARSENAL ZIARANI MAREKANI

**LOS ANGELES,** Marekani

ARSENAL imetangaza kikosi chao cha wachezaji 26 kwa ajili ya ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, huku nahodha Martin Ødegaard na Gabriel Jesus wakitarajiwa kuwa sehemu ya wasafiri.

Klabu hiyo ya London Kaskazini inaanza ziara yake mjini Los Angeles, ambapo itamenyana na Bournemouth Julai 24 na kufuatiwa na mchezo dhidi ya Manchester United Julai 27 kwenye Uwanja wa Sofi huko Inglewood, California.

**Watamaliza safari yao kwa mechi dhidi ya Liverpool huko Philadelphia Julai 31, mwaka huu.**

### ●●● Ni wakati Rice, Ramsdale, Saka na Saliba kuongezewa muda wa...

Jurrien Timber, ambaye alikosa takriban msimu mzima uliopita kutokana na majeraha, ameitwa kwenye kikosi.

Leandro Trossard, Jorginho, Jakub Kiwior na Oleksandr Zinchenko watakuwa sehemu ya kikosi pia licha ya kutoka kwenye Euro 2024 hivi karibuni.

Gabriel Magalhaes, Gabriel Martinelli na Kai Havertz watajiunga na kikosi kuanzia Julai 25, mwaka huu.

Wakati huohuo, Declan Rice, Aaron Ramsdale, Bukayo Saka, David Raya na William Saliba wameongezewa mapumziko kutokana na kuhusika katika hatua za mwisho za Euro 2024 na hawatashiriki kwenye ziara hiyo. Aidha, baada ya kurejea kutoka Marekani, Arsenal wanaendelea na maandalizi yao ya kabla ya msimu mpya kwa kucheza mechi za kirafiki, dhidi ya Bayer Leverkusen na Lyon hapo Emirates Agosti mwaka huu.

Wataanza kampeni yao za Ligi Kuu England Agosti 17, mwaka huu dhidi ya Wolves.



# MARQUEZ KUCHUKUA MIKOBA KOCHA MEXICO

**MEXICO CITY,** Mexico

RAFA Marquez na Shirikisho la Soka la Mexico, wako mbioni kukamilisha mpango wa kocha huyo wa Barcelona B kuwa msaidizi wa Javier Aguirre katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Mexico, vyanzo vimeiambia ESPN.

Marquez mwenye umri wa miaka 45, atahudumu kama kocha msaidizi wa Aguirre kwa miaka miwili ya kwanza ya mkataba kabla ya kumrithi kama kocha mkuu baada ya Kombe la Dunia la 2026.

Hapo awali alikuwa mgombea wa kocha mkuu wa kikosi cha kwanza cha Barcelona kabla ya kuondoka kwa Xavi Aprili, mwaka huu.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba mkataba wa miaka sita na Mexico "Uko karibu sana" kukamilika na kwamba Barcelona wanafahamu hali hiyo.

Marquez alikuwa ameiarifu klabu hiyo ya Katalunya siku chache zilizopita kwamba angezingatia pendekezo la Mexico licha ya kujitolea hivi karibuni kwa Barcelona B hadi Juni 2025.

Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Mexico alikuwa na mapendekezo mengine, lakini aliamua kuongeza mkataba wake Barcelona Juni kutokana na msimu ambao alikaribia kupanda daraja la pili.



# Kocha aonya usajili kwa Toney

**LONDON,** England

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank amezionya klabu zinazomtaka mshambuliaji Ivan Toney kwamba lazima ziwe tayari kulipa bei yake 'ghali' ikiwa zinataka saini yake msimu huu wa majira ya joto.

Toney, ambaye alionesha kiwango kizuri kwenye michuano ya Euro 2024 akiwa sehemu ya kikosi cha Gareth Southgate cha England, amezivutia klabu kadhaa za Ligi Kuu England kama vile Arsenal, Tottenham Hotspur na Chelsea zote zimeonesha nia ya kumtaka fowadi huyo.

Lakini kocha wa 'Nyuki' hao, Frank amekiri kwamba hatamtoa straika wake nyota kirahisi, akithibitisha kuwa angependa kuona mfungaji huyo akisalia Magharibi mwa London.

"Yeye ni mchezaji wa Brentford na ningependa abaki," alisema Frank akiiambia Sky Sports.

"Lakini sijakutana na kocha ambaye hataki wachezaji wengi wazuri iwezekanavyo. Kwa sasa, Ivan ni mchezaji wa Brentford. Najua anafurahia muda wake anaostahili kupumzika baada ya kuitumikia Timu ya Taifa ya England.

"Ningefurahi zaidi kama angebaki nasi. Yeye ni mfungaji mabao na hiyo ni nzuri sana kuwa naye katika timu yako hivyo ukitaka kumnunua ni ghali."

Toney, ambaye alisajiliwa kwa mara ya kwanza na timu hiyo mwaka 2020 baada ya kuondoka Peterborough, amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa.

Hapo awali iliripotiwa kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, aliichezea Brentford mechi 17 pekee msimu wa 2023/24 baada ya kutumikia adhabu ya kufungiwa kwa muda mrefu.

# Ten Hag aipongeza klabu kwa usajili

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amesema wapo mstari wa mbele katika soko la usajili kutokana na uongozi wa klabu hiyo kuchukua hatua za haraka na madhubuti ili kupata wachezaji wapya baada ya usajili wa Leny Yoro na Joshua Zirkzee.

Tangu bilionea wa Uingereza na Mwenyekiti wa INEOS, Sir Jim Ratcliffe, kuchukua udhibiti wa uendeshaji wa soka hapo Old Trafford baada ya kupata hisa asilimia 25 Februari, mwaka huu. United si tu imeshuhudia uongozi mpya, lakini pia kunufaika na mawazo mapya.

United ilimsaini mlinzi wa Ufaransa Yoro kwa mkataba wa miaka mitano kwa ada ya Euro milioni 62. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alikuwa akiwindwa na klabu kadhaa za juu za Ulaya kabla ya kuhamia Manchester, ikiwa ni pamoja na Real Madrid.

Usajili mwingine muhimu ulikuwa ni wa mshambuliaji Zirkzee, ambaye alikuwa na msimu mzuri na Klabu ya Bologna ya Serie A, msimu uliopita na aliichezea Uholanzi katika michuano ya Ulaya. United ililipa Euro milioni 42.5 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kwa mkataba wa miaka mitano.

"Ni vizuri sana kwamba, sisi pia tuko kwenye mstari wa mbele vilevile tuko makini sana," alisema Ten Hag.

"Kwa hiyo, uongozi unafanya kazi nzuri kwa wakati huu na ndivyo tunavyopaswa kufanya kama United."

"Tuna tamaa kubwa na tunapaswa kuwa mstari wa mbele, na kuwa tayari kwa msimu huu. Kadri unavyoiingiza wachezaji wako ndani ndipo tutaweza kufanya kazi kwenye timu yako."



# HABARI MICHEZO

## Simba yawafuata simba Mikumi kuzindua wiki yao

INATOKA UK. 24

nchini ambayo yamejipatia umaarufu kiasi cha klabu nyingi kwa sasa Afrika Mashariki na Kati kuiga.

Wakati huo huo, Klabu ya Simba imemrejesha kikosini Rweyemamu kuendelea na majukumu yake ya kuwa meneja wa timu hiyo.

Habari zilizopatikana jana jijini Dar es Salaam ndani ya klabu hiyo zinasema, Rweyemamu ambaye aliondolewa mwaka jana na kuwa Mkuu wa Programu za Soka la Vijana, alitarajiwa kuondoka jana kuelekea Misri kujiunga na kambi ya timu hiyo iliyoanza Julai 8, mwaka huu, kwenye mji wa Ismailia.

Anachukua nafasi ya Mikael Igendia raia wa Kenya ambaye alikuwa Meneja wa Simba na Mkuu wa Sayansi ya Michezo ambaye aliichukua nafasi yake kabla ya kurejeshwa.

## Yanga yawaonya Duke, Andambwile

INATOKA UK. 24

hakikisha wanaelekeza nguvu na akili zao kwenye lengo mama la kufanya vema mazoezi na kuiletea timu manufaa.

"Haya yanayoendelea kwenye mitandao yanaweza kuwafanya wakabweteka na baadaye wasifanye vizuri, kwetu sisi hayana umuhimu na hatuyaangalii, tunataka atimize majukumu yake uwanjani, hayo ya 'kutrendi' tunawaachia watu wa mitandaoni," alisema Harrison.

Alisema imetokea mara nyingi kwenye soka la Tanzania, baadhi ya wachezaji wanapopata sifa hasa wanapoingia kwenye klabu kubwa, muda mfupi tu baadaye wanabadilika, hivyo wameanza kuwajenga kisaikolojia ili mambo hayo yasiwaathiri kwenye viwango vyao.

Meneja huyo alisema baada ya mechi hiyo, wachezaji wa Yanga wameendelea na mazoezi, ambapo asubuhi wanafanya ya uwanjani na jioni kwenda 'gym', kabla ya mechi yao ya kesho ya Kombe la Mpumalanga dhidi ya TS Galaxy.

Kuhusu mchezaji Shadrack Boka ambaye aliumia kwenye mchezo huo, alisema anaendelea na matibabu na kama hali itaendelea kama ilivyo basi atapelekwa kwenye vipimo ya uchunguzi zaidi.

Baada ya mechi ya kesho, Yanga itamaliza ziara yake Sauzi, Jumapili itakapocheza dhidi ya kwa Kaizer Chiefs, mechi ya Kombe la Toyota, kwenye Uwanja wa Bloemfontein.

# WASHINDI WA DODOMA MARATHON KUIWAKILISHA TANZANIA KIMATAIFA

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesisitiza dhamira yake ya kutumia mbio za Dodoma Marathon kama chanzo cha kuwapata wanariadha sahihi watakaoliwakilisha taifa kwenye mashindano ya kimataifa yakiwamo ya Olimpiki na yale ya Jumuiya ya Madola (Commonwealth).

**Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amebainisha dhamira hiyo ya serikali jijini Dar es Salaam jana huku akithibitisha nia yake ya kukimbia Km 42 (full marathon) kwenye mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika jijini Dodoma Jumapili wiki hii.**

Lengo kuu la mbio hizo zinazotarajiwa kuongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ni kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana akiwa sambamba na mwenyeji wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, Dk. Ndumbaro pamoja na kusifia jitihada za benki hiyo katika kuinua sekta ya michezo nchini, alisema kwa sasa taifa linakabiliwa na uhaba mkubwa wa wanariadha wenye sifa ya kushiriki mashindano ya kimataifa, hivyo serikali imejipanga kutumia mbio hizo kutambua wanariadha wenye sifa sahihi kwa ajili ya maandalizi ya mashindano mbalimbali ya kimataifa.

"Kwa sasa kwenye mashindano ya Olimpiki tunakwenda na wanariadha wachache sana kwa sababu hatuna maandalizi ya kutosha. Hivyo Dodoma Marathon ni moja ya chanzo cha kupata wanariadha wazuri ili baada ya mbio hizi tuweze kuwatambua na kuwapa mafunzo zaidi ili mashindano yajayo ya 'Commonwealth' na Olimpiki na mengine mbalimbali ya kimataifa tuwe na wanariadha wengi zaidi," alibainisha Dk. Ndumbaro huku akipongeza maandalizi ya mbio yenye kuzingatia viwango vya kimataifa.

"Tofauti na mbio hizi, jitihada za NBC kwenye kuinua sekta ya michezo zinaonekana kupitia udhamini wake kwenye Ligi Kuu (Premier League), Championship na Youth League ambapo imewekeza kiasi cha Sh. bilioni 32.6 kwenye ligi hizo.

"Pia benki hii inashiriki katika uwezeshaji kiuchumi kwa wasanii kupitia mfuko wa maendeleo ya sanaa nchini sambamba na kusimamia Kamati ya Hamasa ya Timu za Taifa ambapo mpaka sasa imeshakusanya kiasi cha Sh. bilioni mbili kutokana na ahadi za awali za Sh. bilioni nne zilizopokelewa katika hafla ya uzinduzi wa kamati hiyo," alisema.

Awali akizungumza kwenye mkutano huo, Sabi alisema jitihada za benki hiyo katika kuendeleza sekta ya michezo nchini kwa kiasi kikubwa inachagizwa na imani ya benki hiyo kuwa sanaa na michezo ni nguzo ya ajira na kuunganisha taifa.

"Kwa mfano kupitia udhamini wetu kwenye ligi tatu muhimu za mpira wa miguu hapa nchini, mbali na kuzalisha vipaji tumezalisha ajira za moja kwa moja zaidi ya 7,000 na mamilioni ya ajira zingine kwenye mnyororo wa uchumi.

"Zaidi pia kupitia mbio hizi za Dodoma Marathon kwa kushirikiana na wadau wetu mbalimbali tunalenga kukusanya fedha kusaidia juhudi za serikali katika kuboresha afya ya mama na mtoto kupitia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake na kutoa ufadhili kwa wakunga," alisema.

## 'OOOH YES'...



Jordi Alba akishangilia baada ya kuifungia Inter Miami bao la ushindi wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Chicago Fire juzi kwenye Ligi ya Marekani (Major League Soccer), MLS. **PICHA: MTANDAO**

# *Azam yaahidi kurejea na soka la kuvutia*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Azam FC, amewaahidi mashabiki wa Azam soka la kuvutia kutoka nchini Morocco ambako amekuta timu nyingi zinapenda kuuchezea mpira.

Akizungumza kutoka nchini humo ambako kikosi cha timu hiyo kimepiga kambi kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano, Bruno Ferry, amesema ameona aina fulani ya soka nchini humo ambalo ni la kuvutia na ameanza kuliingiza kwenye kikosi chake kwani kina baadhi ya wachezaji ambao ni mafundi wa mpira miguuni.

"Nimeona soka la Morocco ni la kiufundi sana, wanapenda kuchezea mpira, nasi hatuna tatizo na hilo, tunao wachezaji ambao wanaweza kulicheza, kuna vitu ambavyo tunawaongezea wachezaji wetu ili waweze kucheza aina hiyo ya soka la kuburudisha na kuvutia machoni, huku wakisaka ushindi," alisema kocha huyo.

Jumamosi iliyopita, Azam FC, ilicheza mchezo wa kwanza wa kujipima nguvu dhidi ya US Yacoub Al Mansour inayoshiriki Ligi Daraja la Tatu nchini humo na kushinda mabao 3-0.

Akizungumzia maandalizi kwa ujumla, alisema bado wachezaji wake hawajafika anapopataka, lakini kazi inaendelea kuwafua ili wawe vizuri.

"Bado hatujafika tunapotaka, ila ni hali ya kawaida katika kipindi hiki cha maandalizi, kwa sasa ni muhimu kuendelea na mazoezi ya utimamu wa mwili, ni wakati wa kujiandaa na michezo mbalimbali na kuhakikisha wachezaji wapya wanaingia kwenye mfumo.

"Katika soka kuna hasi na chanya, tunajua kila kitu hakiwezi kuwa sawa na vile unavyotaka, vinahitaji muda, nadhani mashindano yatakapoanza tutakuwa tayari," alisema.

Mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam inajiandaa pia na Ligi ya Mabingwa Afrika, ilipangwa kucheza dhidi ya APR ya Rwanda kuanzia Agosti 16 na 18, mwaka huu kabla ya hapo inatakiwa kuikabili Coastal Union, Agosti 8 katika mechi ya Ngao ya Jamii, Uwanja wa New Amaan Complex, mjini Zanzibar.

# Michezo

Jumanne Julai 23, 2024

Nipashe




## Ten Hag aipongeza klabu kwa usajili

UKURASA 22



Kiungo wa Kati wa Yanga, Duke Abuya, akiwa mazoezini wakati wakiendelea kujiandaa na mechi ya kesho ya Kombe la Mpumalanga dhidi ya TS Galaxy FC ya Afrika Kusini. Katika mechi iliyopita dhidi ya Augsburg, Duke alionyesha kiwango cha juu. **PICHA: YANGA**

## Yanga yawaonya Duke, Andambwile

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewapa angalizo wachezaji wake wapya ambao wameonekana kung'ara katika mechi dhidi ya Augsburg ya Ujerumani kuwa makini na sifa zinazotolewa na mashabiki na mitandao ya kijamii kwani zinaweza kuwaharibu na kupoteza ubora wao.

Wachezaji waliosifiwa zaidi katika mchezo huo uliochezwa Jumamosi iliyopita kweye Uwanja wa Mbombela na Yanga kulala kwa mabao 2-1, ni Duke Abuya, Mkenya aliyesajiliwa kutoka Singida Black Stars na Aziz Ambambwile ambaye pia ni mchezaji mpya kutokea Singida Fountain Gate.

Pamoja na kuangukia kichapo hicho, wachezaji hao waliotokea benchi walionyesha viwango vya hali ya juu na kuibadilisha timu kipindi cha pili.

Akizungumza jana kutoka nchini Afrika Kusini



ambako timu hiyo ipo kwa michezo kadhaa ya kirafiki ya kimataifa, Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, alisema baada ya mechi hiyo na baadhi ya wachezaji kuonyesha viwango vya juu, wamekuwa wakimwagiwa sifa kemkemu, hasa kwenye baadhi ya vyombo vya habari na mitandaoya kijamii.

Alisema wamewapa angalizo wachezaji wao akili zao wasizipeleke huko, bali waelekeze kwenye mafunzo ya mwalimu Miguel Gamondi na kufanya kile ambacho kimewaleta Yanga.

"Hatutaki sana wachezaji wetu wapya yawaingie mambo ya kwenye mitandao ya kijamii, hasa ya kusifiwa kwa sababu yanaweza kuwatoa mchezoni, tunachotaka ku-

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yawafuata simba Mikumi kuzindua wiki yao

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

## ●●● Yatangaza kuiona Simba Day buku tano tu, huku ikimrejesha tena Rweyemamu kuwa meneja wa...

HUKU ikimrejesha meneja wake wa zamani, Patrick Rweyemamu, katika nafasi hiyo, Klabu ya Simba kesho inatarajia kuzindua wiki ya tamasha lao la kila mwaka lijulikanalo kama, Simba Day, kwenye Hifadhi ya Mbuga za Wanyama, Mikumi mkoani Morogoro.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Iman Kajula, alisema wameamua kwenda kuzindua wiki yao mkoani Morogoro kutokana na kutambua kuwa wao kama Watanzania wana jukumu la kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini.**

"Sisi kama Simba tunafahamu jukumu la kutangaza utalii kwani Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii, vile vile tunaunga mkono serikali kutangaza utalii wetu," alisema Kajula.

Naye Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Mikumi, Agustino Masesa, aliishukuru Simba kwa heshima waliyowapa kwenda kuzindua wiki yao katika hifadhi hiyo ambayo Agosti 7, mwaka huu, inafikisha miaka 60.

Akielezea utaratibu mzima wa uzinduzi huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alibainisha kuwa wanachama na mashabiki wa Simba watasafiri kwenda Morogoro na treni ya umeme (SGR), alfajiri siku ya uzinduzi (leo).

"Tumetenga mabehewa matatu maalum kwa ajili ya mashabiki wetu na kila shabiki atasafiri bure hakutakuwa na malipo yoyote kwa ajili ya safari hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema kuingia kwenye hifadhi kila shabiki atalipia kiasi cha shilingi 5,900 kwa ajili ya kuingia ndani ya Hifadhi ya Utalii Mikumi kuangalia wanyama.

Aidha, alitangaza viingilio vya kuingia uwanjani kuangalia mchezo wao, Simba Day dhidi ya APR (Rwanda) kuwa mzunguko ni Sh. 5,000, machungwa Sh. 10,000, VIPC Sh. 20,000, VIP B Sh. 30,000 VIP A Sh. 40,000, pamoja Platinum ambayo ni Sh. 200,000, huku akiweka wazi kuwa tiketi zimeanza kuuzwa tangu jana.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini (TRC), Masanja Kadogosa, aliishukuru Klabu ya Simba kwa kuamua kusafirisha wanachama na mashabiki wake kwa usafiri huo kwani itawapa faida kubwa sana kibiashara kwa kuwa tukio litaangalia na mamilioni ya watu nchini na nje ya nchi.

"Tutashirikiana na watu wote wanaotaka kwenda na kurudi Morogoro na hata ukiangalia nauli zetu ni rafiki Sh. 13,000 tu. Tunawashukuru sana kwa tukio hili, ni tukio la kizalendo, kwa sisi SGR ni jambo kubwa sana kubwa tunahitaji kuonekana," alisema Mkurugenzi huyo.

Uzinduzi huo ni kuelekea kwenye kilele cha tamasha la 16 la Simba Day, ambapo huanza kwa wiki nzima wanachama na mashabiki katika matawi yote nchini kufanya kazi za kujitolea kwa jamii na kutoa misaada mbalimbali kwa wahitaji, kabla ya siku husika ambapo mwaka huu itakuwa ni Agosti 3.

Siku ya kilele mashabiki na wanachama hukusanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa tangu asubuhi ambako huwa na burudani mbalimbali, wasanii, muziki, ngoma, na michezo mbalimbali, ikiwamo kutambulishwa kwa kikosi kipya cha timu hiyo, kabla ya kuhitimisha kuingia uwanjani kucheza mechi, na mwaka huu itakipiga dhidi ya APR ya Rwanda.

Tamasha hilo lilianzishwa 2009, chini ya uongozi wa Hassan Dalali, na limebaki kuwa moja ya matukio makubwa ya kila mwaka

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >